# Nipashe

Jumatatu Oktoba 26, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580380

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




**JPM,** Lissu na Maganja kampeni za lala salama

UKURASA 2

**MAZRUI** adaiwa kutekwa, afunguka

UKURASA 4


FURSA

Mawakala na wasambazaji wa uuzaji Magazeti

Kwa Maombi na Ufafanuzi zaidi Wasiliana nasi

Meneja Usambazaji na Masoko
Mikocheni Light Industrial Area
S.L.P 31042,
Dar es Salaam,
Tanzania

Namba :+255716500500
Barua Pepe: circulation@guardian.co.tz
Mwisho wa Maombi ni 27 Oktoba 2020


# NEC yatangaza siku ya mawakala kupewa barua

• **Yasema** haijapokea malalamiko...*Endelea uk.4*






Mgombea urais kupitia Chama cha ADC, Queen Sendiga, akizungumza na wananchi wa Kata ya Michungwani, Jimbo la Handeni Vijijini, mkoani Tanga wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

## Maalim Seif na Mwinyi wamaliza kampeni kwa kishindo

UKURASA 8




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## Hayati Dk. Mengi atunukiwa tuzo

UKURASA 3


MICHEZO **MASHABIKI MADRID, BARCA WAZAWADIWA** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mgombea urais NCCR kufuta sheria kandamizi

**Na Timothy Itembe,** MARA

MGOMBEA urais kupitia NCCR-Mageuzi, Jeremiah Maganja, ameahidi kubadilisha sheria kandamizi kwa jamii endapo atashinda uchaguzi huu na kuwa rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alitoa ahadi hiyo jana katika mkutano wa kampeni Jimbo la Tarime Mjini mkoani Mara wakati akiomba kura.

Alisema akipatiwa ridhaa na wapigakura ataenda kubadilisha sheria zinazoonekana kuwa kandamizi kwa ustawi wa wananchi, huku akiboresha uchumi wa taifa na kutengeneza mazingira rafiki kwa mfanyabiashara.

Mganja aliongeza kuwa atahakikisha anaimarisha Muungano wa Tanzania na Zanzibar, na kuondoa kero ndogo ndogo zinazokwamisha kufikia maendeleo ndani ya muungano huo.

"Mimi mkinipa ridhaa ya kuwa Rais nitasimamia mchakato wa katiba mpya ya Jaji Joseph Sinde Waryoba ambayo itashirikisha wananchi kutoa maoni, ili kukamilika na kutumika, nitasimamia kuboresha elimu na miundombinu yake ili wanafunzi wakapate elimu bora," alisema na kuendelea:

"Pia nitaenda kufuta michango iliyo kero kwa wazazi na walezi, na wanafunzi watasoma bure msingi hadi chuo, nitahakikisha walimu wanaenda semina za mara kwa mara kukabiliana na mitaala ya kisayansi kadiri inavyokuja, nitahakikisha ninaboresha uchumi wa Taifa hili ili kila mfanyabiashara na Mtanzania kunufaika na rasilimali zilizopo."

Kuhusu afya, Maganja alisema kuwa atafuta vitambulisho vya bima ya afya kwa sababu amegundua kuwa wengi walio na kadi ya vitambulisho hivyo hawanufaiki na matibabu, badala yake wanaambiwa kwenda kununua dawa madukani, huku bima hizo zikibagua baadhi ya magonjwa ya kutibu.

Naye mgombea ubunge wa NCCR Mageuzi Jimbo la Tarime Mjini, Mery Nyagabona, alisema kuwa akipewa ridhaa ya kuwa mbunge atajenga hoja ya kujenga soko ambalo limebomolewa ili wafanyabiashara waende kufanya biashara upya na kukuza mitaji na uchumi wa halmashauri.



Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Moshi, Nathaniel Mshana, akimkabidhi Mkurugenzi wa Kampuni za IPP, Abdiel Mengi, tuzo ya kutambua mchango wa hayati Dk. Regnald Mengi kwa kuongoza mapambano ya kutokomeza ugonjwa wa polio nchini. Tuzo hiyo ilitolewa juzi na Rotary International kupitia Rotary Club ya Moshi. Habari Uk. 3. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# JPM aahidi kumaliza rushwa

**Na Gwamaka Alipipi,** MANYARA

MGOMBEA urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli, amewahakikishia Watanzania kumaliza tatizo la rushwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo na maskini kupata haki zao.

Vilevile, ameahidi kuwatetea wananchi waliopokwa ardhi, kinamama waliodhulumiwa hati, pamoja na kumaliza viporo ambavyo hajavitekeleza.

Aliyasema hayo jana wakati akiwa katika Uwanja wa Kwaraa, wilayani Babati mkoani Manyara, wakati akizungumza na wananchi na wanachama wa CCM waliojitokeza kumsikiliza akiomba kura ya kuchaguliwa kwa mara ya pili kuwa rais.

"Katika kipindi cha miaka mitano tumefanikiwa kupambana na vitendo vya rushwa, wizi pamoja na mali za umma, rushwa ilitapakaa kila idara, tukasema ndani ya miaka mitano lazima tutokomeze," alisema Dk. Magufuli na kuongeza:

"Najua bado rushwa haijaisha, sasa naomba miaka mingine mitano nikaitokomeze, nataka watu maskini wapate haki zao, wengine wamedhulumiwa ardhi, kinamama waliopokwa hati zao, nataka hayo yote yakaishe," alisema.

Aliwataka Watanzania kukataa wagombea wanaohubiri na kutaka Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uvunjike.

Alisema moja ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano ni kudumishwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao umedumu kwa takribani miaka 56.

Pia, alisema serikali imedumisha na kuitunza amani, ambayo ilijengwa tangu utawala wa hayati Mwalimu Julius Nyerere, pamoja na kuhudumisha uhuru.

"Tanzania imekuwa ni kisiwa cha amani kwa mataifa mengi kukimbilia hapa, tumefanikiwa kudumisha amani ambayo iliasisiwa na Mwalimu Julius Nyerere."

Alisema kwenye sekta ya afya, serikali imefanikiwa kujenga hospitali za wilaya 99 katika kipindi cha miaka mitano, zahanati 1,198, vituo vya afya 487, hospitali za mkoa 10 pamoja na hospitali za rufani tatu.

Kadhalika, aliwataka Watanzania wakati wa upigaji kura kuwachagua viongozi wanaotunza tunu za nchi, kwamba mwenye sifa hiyo ni yeye (Dk. Magufuli).

Vilevile, alisema katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, CCM kitaibuka na ushindi mkubwa wa kimbunga, kutokana na idadi kubwa ya wananchi kuhudhuria mikutano ya kampeni.

"Ushindi wa mwaka huu ni kimbunga, kila nilipokuwa nafika katika mikutano ya kampeni nakuta watu wamejaa, nilipokuwa naingia Manyara nilipofika eneo la Minjingu nikakuta watu wengi, hata nilipofika Magugu nikadhani nimeingia makao makuu ya wilaya," alisema Dk. Magufuli.

Aliahidi katika kipindi kijacho, serikali imeweka mkakati wa kuziendeleza bandari, kununua vichwa 36 vya treni pamoja na mabehewa 800.

Kuhusu Mkoa wa Manyara, Dk. Magufuli alisema miaka mitano ijayo serikali itatua kero ya ukosefu wa maji, umeme, ujenzi wa barabara kutoka Babati hadi Kiteto.

Vile vile, aliahidi ujenzi wa barabara za ndani, mitaro, ujenzi wa viwanda, kuajiri wataalamu wa afya, kufuta mashamba ya wawekezaji ambayo hayajaendelezwa, kutatua mgogoro wa ardhi baina ya wakazi na hifadhi ya Ziwa Manyara, pamoja na ujenzi wa stendi ya kisasa.

# Lissu aahidi kuubadili mfumo wa elimu

**Na Christina Mwakangale**

MGOMBEA urais wa CHADEMA, Tundu Lissu, amesema kuwa iwapo atachaguliwa kuwa rais wa Tanzania, atabadili mfumo wa elimu kwa kuhakikisha zinajengwa shule mpya, vyoo pamoja na nyumba za walimu.

Lissu aliyasema haya kwenye mkutano wa kampeni mjini Songea mkoani Ruvuma, akisema pamoja mwamko serikali kutolewa wa uandikishaji wanafunzi shuleni, ujenzi wa miundombinu umekuwa duni kuendana na ongezeko la wanafunzi.

"Madarasa ya shule za msingi hasa mijini yamefurika wanafunzi, darasa ambalo wizara ya elimu inasema ni wanafunzi wastani 45, kuna madarasa ya wanafunzi 200, 150 au 100.

Kwa sababu tumepanua wigo wa kuingiza wanafunzi shuleni, hatujajenga madarasa, hatujajenga shule mpya na vyoo vya walimu, vyoo tulivyonavyo ni vya enzi ya Mwalimu," alisema Lissu na kuongeza kuwa wana mpango mkubwa wa kufanya mabadiliko kwenye elimu yetu.

Alisema mabadiliko katika elimu yatakwenda sambamba na kubadili mtazamo wa elimu kwamba baadhi ya wazazi akitaka kumpeleka mwanawe shuleni, huangalia inayofaulisha.

"Sasa hivi mzazi ukitaka kumpeleka mtoto wako sekondari unajiuliza shule ipi inapasisha, tunachoangalia ni kupasi mitihani, akiwa shule msingi tunampeleka 'tution' (masomo ya ziada) sekondari 'tution', chuo kikuu 'tution'," alisema na kuongeza: "Falsafa hii imejenga taifa la watoto wanaofaulu mitihani na si kufaulu maisha, kuajiriwa popote duniani...hii inawezekana, lazima tubadili mfumo wa elimu ili tusiwe na taifa la wenye ufaulu tu, bali watu wenye maarifa."

Alisema mfumo ulipo unawafanya wahitimu wa Tanzania kuwa na ushindani mdogo kwenye soko la ajira, hususan kwa ukanda wa Afrika Mashariki.

"Yote hii ipo katika mambo makuu, uhuru, haki na maendeleo ya watu."

Aidha, akizungumzia kuhusu sekta afya, Lissu alisema CHADEMA itakaposhinda itahakikisha kila Mtazania anakuwa na bima ya afya, ili kupunguza gharama za matibabu. "Matibabu yana gharama kubwa, fikiria ukilazwa hospitali zetu kwa wiki moja ni shilingi ngapi?" Alihoji.

"Kitu ambacho kinahitajika nchi hii, hakuna mwenye uwezo wa kujitibu mwenyewe hakuna, ugonjwa haubishi hodi kwamba nakuja wiki ijayo.

Bima ya kila mtu itasaidia kwa kuwa hatuugui wote kwa pamoja, ile pesa tuliyochangia itasaidia, tutanunua dawa, tutalipa wauguzi wetu, mchakato utachukua muda, lakini lazima tuanze."

## HABARI KITAIFA

# Hayati Dk. Mengi atunukiwa tuzo

## ■Ni kutambua mchango kutokomeza polio, familia kuendeleza hafla chakula kwa wenye ulemavu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

FAMILIA ya hayati Dk. Regnald Mengi, imesema kuanzia mwaka ujao itaendelea na utaratibu wa kumwenzi baba yao kwa kuandaa hafla ya chakula cha mchana kwa ajili ya watu wenye ulemavu nchini.

Pia, imefafanua kuwa suala la chakula cha mchana kwa watu wenye ulemavu lilikuwa likitekelezwa kama ilivyokuwa desturi miaka yote, Mei 28, mwaka huu, lakini kwa bahati mbaya lilijitokeza tishio la ugonjwa wa virusi vya corona.

Mkurugenzi wa Kampuni ya IPP, Abdiel Mengi, alisema ombi la watu wenye ulemavu kutamani utamaduni huo wa baba yao uenziwe, tayari limeshafanyiwa kazi na Mungu akiwajalia wataendelea nalo mwaka 2021.

Alikuwa akizungumza juzi na watu mbalimbali mjini Moshi, wakati wa hafla ya kupokea tuzo ya 'Paul Harris Fellow Major Donour' iliyotolewa kwa baba yake na Rotary Foundation of Rotary International, kwa ajili ya kutambua mchango wa Dk. Mengi katika kutokomeza ugonjwa wa polio nchini.

Kuna hoja moja aliitoa hapa mzee Elimringi Ngowi: "Nikuhakikishie, mzee (Mengi) hajafa. Kimwili ndio! Kiroho bado yupo. Kama ulivyosema yuko duniani na kupitia kizazi chake na kupitia ndugu, jamaa na marafiki, wote aliowaacha, spirit (roho) yake bado tunaendelea nayo.

"Suala la lunch (chakula) ya wenye ulemavu, lilikuwa litekelezeke kama desturi ilivyokuwa miaka yote, unfortunately (bahati mbaya) mwaka jana tulikuwa tumepanga tuifanye tarehe 28 Mei mwaka huu, na tulikuwa tumeshatangaza kwa viongozi wa taasisi mbalimbali za watu wenye ulemavu, walikuwa wameshapata hiyo taarifa.

"Lakini likaja suala la corona na tukaona mfano kuanzia serikalini, wanasimamisha hadi mbio za Mwenge wa Uhuru na ukishaona hizo dalili ujue situation (hali) ishakuwa serious (mbaya).

"Kwa hiyo tusingeweza kufanya lolote lile kwa muda huo na kuhatarisha maisha ya wenzetu. Ndio maana mwaka jana hukusikia. Lakini mwaka huu tayari limeshafanyiwa kazi. Mwenyenzi Mungu akitujalia mwaka huo unaokuja tutaendelea."

Akishukuru kwa kukabidhiwa tuzo hiyo, Abdiel, alisema familia wanamshukuru mwenyenzi Mungu, kwa kuwa na baba kama Regnald Mengi, kwa sababu alikuwa na vitu vingi sana kwao, na hawana zaidi ya kumshukuru Mungu, kwa namna alivyoweza kumjalia baba yao kuwa na utu unaojali binadamu.

"Na kwa hilo nadhani ni talanta kutoka kwa mwenyenzi Mungu na kila siku tunashukuru kwa kuweza kuwa pembeni yake, kuwa naye, kuwa nyuma yake. Kuna jinsi alivyokuwa anaweza kuitumia hiyo talanta.

"Siku ya leo kupata hii kumbukumbu ni siku ambayo pia inatukumbusha kitu kingine pengine sisi kama wanafamilia. Ni siku ambayo inatukumbusha pia kusema asante kwa mwenyenzi Mungu na kumwombea sala baba yetu, kwa sababu yote haya tunayapata kwa ajili yake.

"Dk. Regnald Mengi alifanya vitu vingi sana katika maisha yake yote, lakini asingeweza kufanya vitu vyote mwenyewe, nyuma yake na pembeni yake alikuwa na watu, alikuwa na taasisi kama hii Rotary Club, ambao pamoja walikuwa wanatiana moyo katika suala zima la kushughulikia changamoto zinazoikabili jamii zetu."

"Niseme tu Rotary mmepiga hatua kubwa sana katika suala zima la kuondoa unnecessary human suffering (kuondoa matatizo yanayowakabili binadamu), hasa suala zima la kuondoa na kufanya ugonjwa wa polio na madhara yake kuonekana katika vitabu vyetu vya historia) ni hatua kubwa sana. Napenda niwapongeze kwa sababu maisha bila polio na hata maradhi mengine kupungua, hayo ni maisha mazuri. Hongereni sana kwa hilo na mafanikio makubwa."

Awali, Rais Rotary Club ya Moshi, Cynthia Asiyo, alisema tuzo hiyo imetolewa kwa niaba ya wanachama wa Rotary Club milioni 1.2 duniani kote, kutambua mchango mkubwa wa Dk. Mengi alioufanya na kuifanya Afrika kuwa haina polio.

Kwa mujibu wa rais huyo, Machi 18, mwaka 2011, Dk. Mengi aliongoza matembezi ya hisani yaliyohusisha mamia ya watu, baada ya kuandaliwa na Rotary Club ya Moshi kuzunguka viunga vya manispaa hiyo na kuchangia peke yake Sh. milioni 40.

Alifafanua kuwa baada ya mchango wa Dk. Mengi, baada ya wiki nane kupita, Afrika nzima ilitangazwa haina ugonjwa wa polio, ndio maana leo wanachama wa Rotary kila mahali na asilimia 90 ya watu wenye utu wote wanamkumbuka Mengi na washirika wake duniani kwa kuondoa ugonjwa huo.

Mkurugenzi wa maduka ya dawa baridi ya binadamu ya Kilimanjaro Pharmacy, Arthur Kiwia, akisoma taarifa ya Siku ya Polio Duniani iliyoandaliwa na Rotary ya Moshi, alisema Tanzania kwa sasa ina club 50 zenye wanachama 750.

**"Suala la lunch (chakula) ya wenye ulemavu, lilikuwa litekelezeke kama desturi ilivyokuwa miaka yote, unfortunately (bahati mbaya) mwaka jana tulikuwa tumepanga tuifanye tarehe 28 Mei mwaka huu, na tulikuwa tumeshatangaza kwa viongozi wa taasisi mbalimbali za watu wenye ulemavu, walikuwa wameshapata hiyo taarifa.**


## KUMBUKUMBU




**Wilneza Mathew Mrema Baba yetu mpendwa,** leo umefikisha miaka minne (4) tangu mwenyezi Mungu alipotwaa roho yako nzuri na kukupa pumziko la milele; hakuna mtu ajuae ni kiasi gani tunaumia mioyoyoni mwetu; hakuna anayejua maumivu ambayo tumejeruhiwa tangu kutwaliwa kwako baba yetu mpenzi; maisha hayajawahi kuwa sawa miyoyoni mwetu kumbukumbu yako inatukumbusha mema yako mazuri kwetu, upendo wa agape na mengi uliotuachia baba; Hakuna siku mpendwa Baba ipitayo bila kufikiria juu yako. Unakumbukwa sana na mke wako mpenzi Eva, watoto wako Lucy, Goodie, Irene, Denis, Monica, Sia, David, Walter, wajukuu wako, Kaka na dada zako, ndugu, jamaa na marafiki pamoja na uongozi na wafanyakazi wa Network Freight Forwarders Ltd.

215956402



## KUPOTOLEWA KWA KADI YA GARI

**SEAWAYS TANZANIA CORPORATION** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **CRANE FORK LIFT** Yenye namba za usajili **T 531 DMZ ,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa

**DAR/MAG/RB/757494 /2020**

115958602



MEDICAL TEAMS International

### Procurement Opportunities

Tender for Framework Agreements

Medical Teams International is Non-Government Organization (NGO) which was founded in 1979, providing life-saving medical care for people in crisis, such as survivors of natural disasters and refugees.

Medical Teams International, Kasulu Tanzania is inviting interested suppliers to express their interest to supply MTI with items per description below. All interested parties are invited to participate.

| | |
|---|---|
| **Procuring Entity:** | Medical Teams International |
| **Tender No:** | MTI20/GEN PROC/001 |
| **Tender Name** | Invitation to Tender for Framework Agreements |
| **Reference Number** | **CATEGORY A: SUPPLY OF GOODS** |
| PP/MTI-TAN/01/2020 | Supply of general stationery. |
| PP/MTI-TAN/02/2020 | Supply of office supplies. |
| PP/MTI-TAN/03/2020 | Supply and maintenance of photocopiers, scanners, computers, printers, Uninterruptible Power Supply (UPS), laptops, software, toners and other ICT accessories. |
| PP/MTI-TAN/04/2020 | Supply of branded items and promotional materials. |
| PP/MTI-TAN/05/2020 | Supply, installation and maintenance of fire and security alarms equipment and security systems. |
| PP/MTI-TAN/06/2020 | Supply of Fuel (Diesel & Petrol) |
| PP/MTI-TAN/07/2020 | Supply of bottled water, dispensing machines and maintenance. |
| PP/MTI-TAN/08/2020 | Supply of motor vehicle/cycle parts and accessories. |
| PP/MTI-TAN/09/2020 | Supply of airtime and scratch cards. |
| PP/MTI-TAN/010/2020 | Supply of office furniture's and fixtures. |
| PP/MTI-TAN/011/2020 | Medicines |
| PP/MTI-TAN/012/2020 | Medical Consumables |
| PP/MTI-TAN/013/2020 | Medical Equipments |
| **Reference Number** | **CATEGORY B: PROVISION OF SERVICES** |
| PP/MTI-TAN/014/2020 | Provision of catering services. |
| PP/MTI-TAN/015/2020 | Provision of air travel, reservations and ticketing services. |
| PP/MTI-TAN/016/2020 | Provision of sanitary, fumigation, pest control and cleaning services. |
| PP/MTI-TAN/017/2020 | Provision of internet services. |
| PP/MTI-TAN/018/2020 | Provision of hotel accommodation and conference facilities. |
| PP/MTI-TAN/019/2020 | Provision of security services (guards, dog patrols and security survey). |
| PP/MTI-TAN/020/2020 | Servicing, repair and maintenance of vehicles and motorcycles |
| PP/MTI-TAN/021/2020 | Vehicle Hire-minibus, pickups, hardtop Landcruiser's |
| PP/MTI-TAN/022/2020 | Provision of printing services |
| **Source of Fund** | Bureau of Population, Refugees and Migration & UNHCR |
| **Eligible Firms** | National (Registered in Tanzania) |
| **Method of Procurement** | National Competitive Bidding |
| **Mode Application** | Via Email; procurementtz@medicalteams.org (Please send an introduction email for document inquiry) |
| **Deadline** | 11th November 2020 4:30PM |
| **Bids Submission** | Effective 12rd October to 11th November 2020 |

*"Daring to love like Jesus, we boldly break barriers to health and restore wholeness in a hurting world"*

215940502

## ...Yataka ushahidi uwapo vituo hewa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imewataka wanasiasa na wagombea wanaodai kuwapo kwa vituo na wapigakura hewa kupeleka ushahidi na endapo wakishindwa kufanya hivyo hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yao.

Akizungumza jana na waandishi wa habari Jijini Dodoma, Mkurugenzi wa Tume hiyo, Dk. Wilson Charles Mahera, alisema tuhuma hizo zinaleta taharuki kwa jambo ambalo si la kweli.

"Jambo hilo ni uongo na uzushi ambao unalenga kuchafua Tume ya uchaguzi na kuchafua mchakato mzima wa uchaguzi ambao umefanyika kwa weledi wa hali ya juu na umetumia gharama kubwa tangu kuanza maandalizi ya daftari la wapigakura, vituo vya kuandikisha wapiga kura, uwekaji wazi wa daftari la wapiga kura, kupata daftari lenyewe,"alisema.

Aidha, alisema vituo vya kupigia kura ni vingi kuliko vya kujiandikishia kwa sababu kila kituo wameweka idadi ya wapigakura wasiopungua 500 ili kurahisisha zoezi la upigaji kura.

"Vituo vilivyotumika kuandikisha wapiga kura vilikuwa 37,814,na vituo vya kupigia kura ni 80,155, hii inatokana na kwamba kwenye kituo kimoja kilichotumika kujiandikisha kinaweza kutoa vituo vitatu kwa sababu kituo kimoja kinatakiwa kuwa na wapiga kura 450 hadi 500," alisema.

Alisema daftari la kudumu la wapiga kura limegharimu Sh. bilioni 157 na uchaguzi utagharimu Sh.Bilioni 331 mbapo hadi sasa zimetumika Sh.Bilioni 276.

"Hawa wanaojaribu kutoa taarifa za uongo na kutaka kuwatisha wananchi wana nia ovu kwa nchi, watu wasitishike na taarifa za mtandaoni kwasababu wapigakura wapo kwenye ground na wanaishi Tanzania wanajua hali halisi ya nchi ilivyo, kwasababu tumepokea simu kutoka nje ya nchi nyingi watu wakidhani huku hakuna amani kabisa kwasababu ya watu wachache mitandaoni wanaochagua hali ya hewa," alisema.

Alisema Tume ikifanya kila hatua kwa kushirikisha vyama vyote na vilikuwa vinaruhusiwa kuweka mawakala kuanzia hatua ya uandikishaji.

"Orodha wanayo na vyama vya siasa pia vinayo lakini hapa kuna orodha ya vituo vya kuandikisha wapigakura, ambapo vile vituo baada ya kuandikisha wapiga kura vinabadilika ambapo kituo cha kuandikishia vinabadilika na kuwa viwili au zaidi," alisema.

Aliongeza: "Na idadi ya vituo tumekabidhi kwa vyama vya siasa wanavyo, na kama mtu anasema kuna vituo hewa avilete na asipopeleka atawajibika kwa maneno yake ya uchochezi pale sheria za nchi zitakapochukua mkondo wake."



Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Wilson Mahera Charles, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) katika ofisi za Tume, jijini Dodoma jana. **PICHA: MROKI MROKI (NEC)**

# NEC kutoa barua za mawakala kesho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema imepanga kutoa barua za utambulisho wa mawakala kesho.

Vile vile, imesema haijapokea taarifa rasmi kutoka kwa wasimamizi wa majimbo kuhusu vyama kulalamika baadhi ya mawakala wake kutoapishwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, alikiri kuwa mawakala hao hawajapewa barua na kuahidi kutolewa kesho (Oktoba 27).

"Mawakala hawajapewa barua kwa kuwa tumepanga zitatolewa Oktoba 27, kwa hiyo zipo kwenye maandalizi, kinachotaka kutokea ni baadhi ya vyama havitaki kufuata taratibu zilizowekwa. Wasimamizi wa uchaguzi ndani ya majimbo tutasikitika sana kama umemwapisha mtu halafu huandai barua yake," alisema.

"Wakumbuke masuala ya kisheria yapo, na ukifanya mambo ya ovyo sio mwisho, haki nyingine zitatafutwa kwa hatua nyingine ni vyema mkazingatia utaratibu."

Kadhalika, Mkurugenzi huyo wa NEC, alisisitiza kuwa matokeo yatatangazwa kwa wakati baada ya watu kumaliza kupiga kura. Kuhusu malalamiko kuwa baadhi ya mawakala hawajaapishwa, alisema: "Hatujapokea taarifa rasmi kwa wasimamizi wa majimbo kuhusu vyama kulalamika baadhi ya mawakala wake kutoapishwa, kuna maeneo tulipigiwa simu na tukashughulikia."

Akizungumzia kampeni, alisema kwa upande wa Tanzania Bara zitahitimishwa Oktoba 27, wakati Zanzibar wanahitimisha leo. "Sasa hivi tuna ratiba ya toleo la sita ambalo ndio la mwisho, kwa hiyo tunataka kusisitiza ratiba hiyo inaangalia maadili ya uchaguzi ya mwaka 2020 kwamba kampeni zinaanza saa mbili asubuhi na kuisha saa 12 jioni," alisema.

Hata hivyo, alisema kuna tatizo la baadhi ya vyama au wagombea kutozingatia muda licha ya kuelezwa, lakini wamekuwa wakaidi.

"Kumekuwa na tatizo kwa baadhi ya vyama kuwazuia wagombea urais wanaopita huko, unakuta mgombea ubunge au diwani anakuwa na mkutano eneo ambalo mgombea urais anapita. Kama mgombea ana mkutano kwenye eneo hilo msimamizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo anatakiwa kusimamisha mikutano ya kampeni kwa wagombea ubunge na udiwani," alisisitiza.

Kadhalika, alisema hakuna nafasi ya kubadili ratiba hiyo na kuwataka wagombea kufuata iliyotolewa kwenye maeneo waliyoamua wenyewe na wazingatie kumaliza saa 12 jioni.

"Wanaosaidia kuratibu kampeni hizo ngazi ya jimbo, waache wagombea wa kiti cha urais na makamu wa rais wafanye kampeni zao kwa amani, kama mgombea anafuata ratiba toleo la sita ukienda nje ya hiyo ndio utakapokumbana na tatizo, usivamie eneo ambalo sio la kwako," alisema.

Akizungumzia vifaa vya kupigia kura, aliwahakikishia Watanzania kuwa Tume imejiandaa vizuri na vifaa vyote muhimu hadi jana jioni vilikuwa vimefika kwenye majimbo yote nchini.

"Na kule jimboni wasimamizi wa uchaguzi wamejipanga vizuri, na sasa wamejipanga kuvisafirisha kupeleka kata na vituo husika, tunawasihi watumie siku ya leo na kesho kutwa kufikisha kwenye vituo ili kusiwe na tatizo la kuchelewesha vifaa," alisema.

Alisisitiza kuwa hakutakuwa na tatizo la vituo vya kupigia kura kuchelewa kufunguliwa saa moja asubuhi siku ya Oktoba 28 na kuwasihi Watanzania wajitokeze ili kupiga kura.

Kwa upande wa vitambulisho, alisisitiza kuwa mpigakura aliyejiandikisha na kupoteza kadi atapiga kwa kitambulisho mbadala vilivyoainishwa na Tume baada ya kuthibitisha kuwa amepoteza.

# Kigogo wa ACT adai kutekwa

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, anadai kutekwa na watu wasiojulikana majira ya asubuhi jana, kisha kujitokeza baadaye na kueleza kilichomtokea.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, aliwataka wanaomshikilia Naibu Katibu Mkuu huyo kumwachia mara moja.

Maalim Seif ambaye ni mgombea urais wa Zanzibar kupitia ACT-Wazalendo, alisema kitendo cha kutekwa kiongozi hakikubaliki wakati utaratibu wa kukamata mtu unaeleweka.

Aidha, alisema hawapo tayari kuvumilia vitendo vyovyote vya uonevu vinavyopangwa kufanywa dhidi yao.

Kwa upande wake Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Awadhi Juma Haji, alisema wamepokea taarifa za kutekwa kwa Naibu Katibu Mkuu huyo wa ACT-Wazalendo Zanzibar, na kwamba taarifa hizo wanazifanyia kazi baadaye watatoa taarifa rasmi.

Nassor Ahmed Mazrui, anadaiwa kuvamiwa na watu wasiojulikana mapema jana asubuhi maeneo ya Saateni, Wilaya ya Mjini, wakati akielekea ofisini kwake Vuga Mjini Zanzibar.

AFUNGUKA

Akizungumza baada ya kuachiwa katika mkutano wa hadhara wa kufungwa kwa kampeni za ACT-Wazalendo jana jioni, Mazrui Nassor ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushindi ya Maalim Seif, alisema: "Ama kwa hakika ilikuwa ni siku ngumu kwangu, lakini nimevumilia kwa sababu ni ukombozi wa Wazanzibari."

"Leo saa mbili kasoro robo asubuhi nilipokuwa natokea Mtoni kuja Vuga kwa ajili ya maandalizi ya mkutano huu, tulipofika kwenye daraja la Sateni, walitokea watu na gari aina ya Prado, wakatugonga kwa nguvu ikatupiga na daraja, ikiwa hatuwezi kwenda mbele wala hatuwezi kurudi nyuma."

"Wakati huo kuna watu walishuka kwenye hilo gari lililotugonga, wakapiga bastola juu na wakapiga kwenye tairi ya gari yangu, mlango wa dereva ukafunguliwa, dereva akavutwa na kutupwa chini, nikawekewa bastola juu ya uso wangu na nikawekewa nyingine sita, nikabebwa hangahanga na kutupwa ndani ya gari na kufunikwa uso wote."

"Nilifunikwa na kukabwa roho kisawasawa, kitambaa cha uso nimekifungua mwenye saa sita na nusu mchana nilipotupwa katika pori la Bweleo.

"Kila mtu lazima alaani vitendo viovu vya kuteka nyara Wazanzibari kwa sababu ni viovu, hizi ni siasa potofu."

TANGAZO


JAZA TUKUJAZE TENA
Nunua kifurushi upate Bonus za Dakika, SMS, MB's na nafasi ya kushinda Simu Janja kila siku.
Piga *147*00#
pia kwa Tigo Rusha au Tigo Pesa
*Vigezo na masharti kuzingatiwa tembelea www.tigo.co.tz
tigo
215959802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF, TPLB malizeni kero hii ratiba Ligi Kuu Bara

**BAADA** ya miamba ya soka nchini, Yanga kushuka Dimba la CCM Kirumba jijini Mwanza jana, kuwavaa wenyeji wao KMC FC, leo kigogo kingine cha kabumbu nchini, Simba kitakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Ruvu Shooting katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, miamba hiyo ya soka nchini, michezo yao hiyo ya jana na leo ni ya raundi ya saba, wakati timu nyingine kuanzia jana juzi na leo zikicheza mechi zao za raundi ya nane katika ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 msimu huu wa 2020/21.

Hatua hiyo inatokana Bodi ya Ligi nchini (TPLB), kuahirisha mechi ya Simba na Yanga ambayo ilitarajiwa kupigwa Oktoba 8, mwaka huu kwa kile ilichoeleza kuwa ni kuhofia wachezaji wa timu hizo ambao walijiunga na timu zao za taifa wakati wa Kalenda ya Fifa, kukwama kuwahi kurejea nchini kutokana na changamoto ya usafiri wa ndege inayotokana na baadhi ya nchi kuwa katika karantini ya mlipuko wa virusi vya corona, COVID-19.

Lakini pamoja na sababu hizo, timu kama Azam FC ambayo nayo baadhi ya wachezaji wake waliitwa katika mataifa yao kwenda kuzitumikia timu zao za taifa, yenyewe haikuahirishiwa mechi zake na ratiba yao ya Ligi Kuu iliendelea kama kawaida.

Kitendo hicho kimezua malalamiko mengi kutoka kwa baadhi ya timu zinazoshiriki Ligi Kuu, kwa kuona vigogo hao wa soka nchini wanabebwa kwa namna moja ama nyingine kutokana na kupata muda mrefu wa kupumzika kuliko timu zingine huku zikiendelea kuviandaa vikosi vyao.

Hata hivyo, katika kipindi hicho tulishuhudia pia miamba hiyo ikionyesha uhitaji wa mechi kwa kucheza michezo ya kirafiki ili kuendelea kuwajengea wachezaji wao utimamu wa kimwili na kupata muunganiko mzuri wa vikosi vyao, jambo ambalo linaonyesha wazi klabu hizo zilihitaji kuendelea kucheza.

Nipashe tunatambua pengine malengo ya TPLB na Shirikisho la Soka nchini (TFF), lilikuwa zuri kwa maslahi mapana ya timu hizo, lakini halikuzingatia usawa na haki kwa timu zingine ili kuondoa malalamiko ya siyo na msingi ambayo yangeweza kupukika.

Hivyo, ni vizuri TPLB kwa kushirikiana na TFF kuepuka lawama ama malalamiko kama haya kwa kuamua mechi zote za Ligi Kuu kusimama wakati wa Kalenda ya Fifa ijayo kwa kuwa bado tunatambua kuna ratiba nyingi za mechi za kimataifa ambazo zitajitokeza ligi hiyo ikiendelea.

Lengo letu ni kutaka kuona mechi zote za raundi moja zikichezwa ndani ya wiki moja kama ilivyo sasa, bila timu nyingine kubaki nyuma kama ambavyo ilivyo sasa wakati mechi hiyo ya watani wa jadi ingewezwa kuchezwa mapema zaidi na kuondoa kiporo hicho. Tunatoa tahadhari hiyo mapema hasa kwa kutambua kuwa mwezi ujao itatoka ratiba ya michuano ya Shirikisho la Soka barani Afrika (Caf) kwa ngazi ya klabu, ambapo Simba na Namungo FC zitaipeperusha bendera ya Tanzania Bara kwenye Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho.

Kwa misimu kadhaa ukiwamo uliopita, tumeshuhudia timu zinazoiwakilisha nchini kwenye michuano hiyo, zikiwa na viporo vingi, hivyo kwa utaratibu huu wa TPLB wa kutengeneza viporo, ni wazi tuendapo kunaweza kuwa na timu ambazo zinabaki nyuma michezo mitatu hadi minne na hivyo kuzisababishia ratiba ngumu kwao.

Lakini pia viporo ndivyo husababisha baadhi ya timu kudaiwa kutumia mwanya huo kuweza kupanga matokeo, jambo ambalo kama ndivyo linaweza kuchangia kukosekana bingwa halali na wawakilishi bora wa nchi kwenye michuano ya kimataifa.

Kwa mantiki hiyo, tunataka kuona TPLB ikijipanga kukabiliana na kalenda za kimataifa bila kusababisha viporo vingi kwa baadhi ya timu kama ambavyo mataifa mengi yaliyopiga hatua kisoka humudu kufanya hivyo pasipo kuathiri ratiba zao za michuano ya ndani, hatua ambayo si tu itaondoa malalamiko kutoka kwa baadhi ya klabu, ila pia itaifanya ligi yetu kuzidi kuwa bora na mwisho wa msimu kumpata bingwa aliyestahili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kwa nini Manula tu na si kocha wa makipa Simba?

**MARA** baada ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Prisons Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga, baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba wamekuwa wakimtolea povu kipa namba moja wa timu hiyo, Aishi Manula kuwa alichangia kwa kiasi kikubwa kupoteza mechi hiyo.

Wanadai kuwa aina ya goli alilofungwa halistahili kwa kipa mkongwe na mzoefu kama yeye, tena akiwa ni namba moja kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars, achilia mbali kwenye klabu hiyo.

Wanasimba wanaomlaumu Manula wanadai kuwa hawalalamiki kwa sababu wamefungwa, bali wanacholalamikia ni aina ya mabao ya kipa huyo anayofungwa kuwa ni yale yale na amekuwa hajirekebishi. Simba imefungwa mbao matatu mpaka sasa kwenye mechi za Ligi Kuu, lakini wanadai mabao mawili ambayo mpaka sasa timu yao imefungwa ni uzembe wa Manula.

Ni hilo dhidi ya Prisons ambalo, Manula alitoka golini bila mahesabu, lakini alipogundua hawezi kuupata mpira alirudi tena nyuma, na tayari Samson Mbangula alikuwa ameshaenda hewani na kuupiga kichwa mpira uliokwenda wavuni goli likiwa tayari tupu.

Bao lingine ni dhidi ya Mtibwa Sugar, Simba ilipopata sare ya 1-1, aina ya goli alilofungwa pia hawakuridhika nalo. Ni kwamba Manula alitoka golini kwenda kuufuata mpira kwenye eneo ambalo hakutakiwa kwenda.

Badala ya kuelekea mbele ili aufikie mpira kabla ya mchezaji, yeye alienda eneo ambalo alikuwa anasubiria mchezaji aukose ili yeye ndio audake.

Haya yote, ukichanganya na baadhi ya makosa ya msimu uliopita, wakijumlisha mpaka yale ya Ligi ya Mabingwa Simba ilipokuwa ikipokea vipigo vya mabao 5-0 ugenini, vimewafanya wanachama na mashabiki wengi wawe na wasiwasi naye, huku timu hiyo ikiwa inakwenda tena kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika yeye akiwa ndiye kipa tegemeo.

Ni ukweli usiopingika Manula amekuwa na makosa mengi binafsi yanayoigharimu timu wakati mwingine. Ni makosa ambayo hayatakiwi kwa kipa mkubwa anayedakia timu kubwa kama ya Simba kuyafanya. Kipa huyo amekuwa dhaifu kwenye mashuti ya mbali, kona, faulo na krosi.

Imefikia hatua wanachama na mashabiki wa Simba timu yao inapopigiwa faulo au kona wanakuwa na wasiwasi. Hii si dalili nzuri kwake. Siku zote, makipa wa timu kubwa ni wale ambao wanaweza kuisaidia timu kwenye nyakati ngumu.

Mfano Simba ilipokuwa na kina Idd Pazi, Mohamed Mwameja au Juma Kaseja. Ni makipa ambao walikuwa na uwezo wa kuifanya timu ishinde kwenye mechi ambayo ilitakiwa itoke sare. Na waliifanya timu itoke sare kwenye mechi ambayo ilitakiwa ifungwe. Hizo ndizo sifa za kipa wa timu kubwa siku zote. Tatizo lingine ninaloliona ni kwamba Manula si jasiri golini. Halitawali goli na kuwafanya washambuliaji kutomhofia.

Wakati wanachama na mashabiki wa Simba wakimjia juu Manula, pamoja na mapungufu yake, lakini nina wasiwasi na Kocha wa Makipa wa Simba Mwarami Mohamed kama anafanya kazi yake sawasawa. Mapungufu mengi ya Manula yameanza kujitokeza akiwa Simba, lakini hayakuwa mengi alivyokuwa Azam FC.

Kwa kuthibitisha hilo hata kipa namba mbili wa timu hiyo, Beno Kakolanya kabla hajajiunga na timu hiyo alikuwa kipa tegemeo wa klabu ya Yanga. Lakini alipojiunga na Simba kwa sasa uwezo wake umepungua na si kama ule aliokuwa nayo alikotoka.

Ukweli ni kwamba makipa wengi, wamekuwa wakishuka uwezo wanapojiunga na Simba tofauti na huko walikotoka. Hii inanipa wasiwasi juu ya mafunzo ya kocha wa makipa ambaye amekuwa akiona uwezo wa makipa wake mara kwa mara ukipungua badala ya kuimarika na hakuna chochote ambacho kimekuwa kikirekebishwa.

Imekuwa rahisi timu inapofanya vibaya lawama kumwangukia kocha mkuu katika klabu husika, hadi kufikia hatua ya kutimuliwa, lakini kipa anapofanya makosa ya kujirudia mara kwa mara na kuigharimu timu, husikii kocha wa makipa akitajwa!

Hivyo, baadhi ya wanachama na mashabiki wa klabu ya Simba wameanza kushinikiza klabu kutafuta kipa mwingine kipindi cha dirisha dogo lakini husikii akitajwa kocha wa makipa! Huku wakitaka kuondolewa kwa Ally Salim ambaye ni kipa wa tatu, wengi wakimpendekeza Daniel Mgore wa Biashara United, lakini binafsi naona hata yeye kama akienda Simba anaweza pia kushuka kiwango kama benchi la ufundi halitoongezwa wataalamu au makocha wa makipa kwenye kikosi hicho.

Ikumbukwe kuwa kwenye Ligi ya Mabingwa timu nyingi hasa za Afrika Kaskazini maarufu kama za Waarabu, ni wazuri sana kwenye faulo, krosi na kona, hivyo kama kocha wa makipa na Manula hawatokuwa makini wanaweza kuwapa wakati mgumu wachezaji wengine wa Simba, wanachama na mashabiki wao.

**TANGAZO**

MCB BANK — BETTER TOGETHER

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2020 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Sept-2020 | Robo Mwaka iliyopita 31-Jun-2020 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 514 | 141 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 5,290 | 2,621 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 49 | 281 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 24 | - |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | 268 | 132 |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 4,000 | 1,000 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 15,766 | 15,347 |
| 12. Mali Nyingine | 4,867 | 5,213 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,037 | 1,046 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **31,814** | **25,781** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18. Amana za Wateja | 15,802 | 8,926 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 836 | 616 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 294 | 421 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | 281 | 222 |
| 27. Dhima Nyingine | 1,215 | 1,165 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **18,428** | **11,350** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **13,387** | **14,431** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30,912 | 30,912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (14,445) | (14,555) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (3,080) | (1,926) |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **13,387** | **14,431** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 296 | 300 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | (266) | (266) |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 42% | 56% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.8% | 1.9% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 98% | 169% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 49% | 58% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 62% | 63% |
| - Ongezeko la Amana | 77% | -15% |
| - Ongezeko la Mali | 23% | -10% |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2020 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo ya Mwaka sasa 30-Sept-2020 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Sept-2019 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sept-2020 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sept-2019 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 639 | 709 | 1,958 | 2,215 |
| 2. Gharama za Riba | 138 | 172 | 360 | 449 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **502** | **537** | **1,599** | **1,766** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (0) | 62 | (25) | (53) |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 75 | 169 | 196 | 311 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | 0 | 12 | 6 | 21 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 69 | 157 | 181 | 289 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 6 | - | 9 | 1 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 1,731 | 2,161 | 4,901 | 6,157 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 734 | 922 | 2,093 | 2,629 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 997 | 1,239 | 2,808 | 3,528 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,153)** | **(1,517)** | **(3,080)** | **(4,027)** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **(1,153)** | **(1,517)** | **(3,080)** | **(4,027)** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,153)** | **(1,517)** | **(3,080)** | **(4,027)** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 62 | 56 | 62 | 56 |
| 14. Mapato kwa Hisa | -19 | -25 | -50 | -65 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | *-4%* | *-5%* | *-11%* | *-14%* |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | *-8%* | *-9%* | *-21%* | *-21%* |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | *300%* | *306%* | *273%* | *296%* |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | *3%* | *3%* | *8%* | *9%* |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2020 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Sept-2020 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sept-2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Sept-2019 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | (1,153) | (975) | (3,080) | (4,027) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara katika Mali | 379 | 319 | 993 | 1,346 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (3,419) | 417 | (2,614) | (199) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 6,876 | (1,600) | 4,729 | 3,711 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 66 | (329) | 50 | 121 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 76 | 472 | 1,067 | (609) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **2,824** | **(1,696)** | **1,144** | **343** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| - Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | - | - | (41) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | 946 |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **-** | **-** | **-** | **905** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | - | - | - | - |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - | - | - |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | 2,824 | (1,696) | 1,144 | 1,248 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 2,957 | 4,653 | 1,557 | 1,557 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 5,781 | 2,957 | 2,702 | 2,805 |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2020 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Ziada nyingine | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (14,445) | - | - | - | 16,467 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (3,080) | - | - | - | (3,080) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada nyingine | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(17,526)** | **-** | **-** | **-** | **13,387** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (9,976) | - | 179 | 179 | 21,294 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (4,827) | - | - | - | (4,827) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | 179 | - | (179) | - | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | 179 | - | - | (179) | (0) |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(14,445)** | **-** | **-** | **(0)** | **16,467** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2020**

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha za robo, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ……………………. (Imesainiwa) | 21 Octoba 2020 |
| Selemani Kijori (Mkuu wa Fedha) | ……………………. (Imesainiwa) | 21 Octoba 2020 |
| Patrick Mashallah (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ……………………. (Imesainiwa) | 21 Octoba 2020 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| 1/ Francis Ramadhani | ……………………. (Imesainiwa) | 21 Octoba 2020 |
| 2/ Celestine Muganga | ……………………. (Imesainiwa) | 21 Octoba 2020 |

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES MADE UNDER REGULATION 11

| S/N. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | **Current Accounts** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 50,000 |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 7,500 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 2,500 for amounts less than 5Mil otherwise 0.1% max TZS 100,000 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | TZS 1,300 |
| | (e) ATM mini statement | TZS 300 |
| | (f) Interim statement per page | TZS 1,500 |
| | (g) Periodic scheduled statement | 0 |
| | (h) Cheque book | TZS 500 per leaf |
| | (i) Dishonoured cheque | TZS 100,000 |
| | (j) Special clearance | n/a |
| | (k) Counter cheque | TZS 6,000 |
| | (l) Stop payment | TZS 40,000 |
| | (m) Standing order (Same bank) | Free |
| | (n) Balance enquiry | TZS 300 |
| | (o) New ATM card issuance | TZS 10,000 |
| | (p) ATM card renewal or replacement (indicate costs for different card types) | TZS 10,000 |
| | (q) Overdrawn account interest charge | 20% |
| | (r) Unarranged overdraft | 20% |
| | (s) Interbank transfer | TZS 10,000 |
| | (t) Bill payments through ATM | n/a |
| | (u) Deposit fee | 0 |
| | (v) Other (please specify) | n/a |
| 2 | **Savings Accounts (Disclose for product specific types)** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 5,000 |
| | (b) Monthly service fee | TZS 1,400 |
| | (c) Interim statement | TZS 1,500 |
| | (d) Account closure | TZS 20,000 |
| 3 | **Electronic Banking** | |
| | (a) Internet banking monthly fee | n/a |
| | (b) Internet transfers | n/a |
| | (c) SMS banking | TZS 1700 |
| | (d) Other | n/a |
| 4 | **Foreign Exchange Transaction** | |
| | (a) Purchase/sale of TCs transactions over the | n/a |
| | (b) Purchase of foreign cheque | n/a |
| | (c) Sale/purchase of cash passport | n/a |
| | (d) Telegraphic transfer | n/a |
| | (e) Telex/SWIFT | n/a |
| | (f) Tranfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank) | 0 |
| 5 | **Personal Loans** | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | 3% |
| | (i) Personal loans | 17% |
| | (ii) Overdrafts | 20% |
| | (iii) Mortgage finance | n/a |
| | (iv) Asset finance | n/a |
| | (b) Unpaid loan instalment | 20% |
| | (d) Valuation fees | n/a |
| | (e) Other | n/a |

**Deposit Rates**

| | Fixed Deposit - TZS | 3 Months | 6 Months | 12 Months |
|---|---|---|---|---|
| | 1 - 2 Mln | 1.5% | 2.5% | 3.5% |
| | 2 - 10Mln | 2.0% | 3.0% | 4.0% |
| | 10 - 50 Mln | 2.5% | 3.5% | 4.5% |
| | 50 - 100 Mln | 3.0% | 4.0% | 5.0% |
| | 100 - 300 Mln | 3.5% | 4.5% | 5.5% |
| | 300 - 500 Mln | 4.0% | 5.0% | 6.0% |
| | 500m - 1Bln | 4.5% | 5.5% | 6.5% |
| | Above 1 Bln | Contact Treasury | | |
| | **Savings Account - TZS** | **Accrue on Daily Cleared balance paid Monthly** | | |
| | 0- 50k | 0.5% | | |
| | 50k - 1mln | 1.0% | | |
| | 1 - 10mln | 1.5% | | |
| | 10 - 100mln | 2.0% | | |
| | Over 1mln | 2.5% | | |

**Base Lending Rates**

| | Loan Type | Base rate | |
|---|---|---|---|
| 1 | Short term (up to 1year) | 19.5% | +/-4.5% |
| 2 | Medium term (2-4 years) | 21.5% | +/-1.5% |
| 4 | Term loans (over 5 years) | 19.0% | +/-4.0% |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Richard L. Makungwa | Chief Executive Officer | | 21 October 2020 |
| 2 | Leticia Ndongole | Ag. Head of Business Development & Marketing | | 21 October 2020 |
| 3 | Selemani Kijori | Head of Finance | | 21 October 2020 |

**Head Office**

**Mlimani Tower - Mezzanine Floor,**
**Sam Nujoma Road**
**P.O.Box 61002,**
**Dar es salaam**
**Phone: 022-2772954/7**
**email: info@mcb.co.tz**
**Customer Care No.:**
**0629331151|0629331755|0800750033**

**Mlimani Branch**
**Mlimani Tower - Ground Floor**
**Sam Nujoma Road**
**Dar es salaam**

**Samora Branch**
**Samora Avenue**
**Consolidated Holding Building Ground Floor**

**Regional Office - Morogoro**
**19, Plot E, Nkomo Street**
**Phone: +255 622 005 574**
**Morogoro**

**Regional Office - Mbeya**
**90, Plot L, Sokomatola Street**
**Phone: +255 766 903 575**
**Mbeya**

**Regional Office - Mwanza**
**18, Plot A, Kirumba Street**
**Phone: +55 788 138 238**
**Mwanza**



## HABARI KITAIFA

## Wakulima mwani wapatiwa vipande vya kamba 700,000

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, amekabidhi vipande vya kamba za manila 700,000 kwa wakulima wa mwani katika Kijiji cha Songosongo, wilayani Kilwa, Mkoa wa Lindi.

Akizungumza na wananchi wa Songosongo juzi, Dk. Tamatamah alisema serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) imetoa kamba hizo ili kuwawezesha wakulima wa mwani kwani kamba ilikuwa ni moja ya changamoto waliyokuwa wakikabiliana nayo.

Kamba hizi za manila (ambazo kila moja ina urefu wa mita 10) katika kilimo cha mwani, hufungwa katika vigingi na hutumika kwa ajili ya kuoteshea mwani, ambapo mwani hufungwa katika kamba hizo zinazosaidia pia mwani kutochukuliwa na maji ya bahari pale panapokuwapo na wimbi.

Dk. Tamatamah alisema duniani kote kwa sasa mwani unalimwa kibiashara, hivyo mwani ni moja ya zao linalopewa kipaumbele katika wizara. Katika kilimo cha mwani wakulima wanakutana na changamoto mbalimbali zikiwamo za ukosefu wa mitaji na masoko.

"Wizara kupitia sekta ya uvuvi imeanza kutoa kamba ambazo ni moja ya pembejeo muhimu kwa wakulima wa mwani ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha wakulima hao kwa kuwapunguzia sehemu ya gharama za uzalishaji ili baadaye waweze kusimama wenyewe," alisema Dk. Tamatamah.

Pia, alisema kama wakulima watalima vizuri katika kamba moja ya mita kumi katika bamvua nne (miezi miwili), wanaweza kupata kati ya kilo 8-10, na kamba hizo walizopewa zinaweza kutumika kwa mwaka mzima. Lengo la wizara ni kusambaza kamba hizi kwa wakulima wa mwani maeneo yote Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa Dk. Tamatamah, ipo changamoto ya soko la mwani hasa kwenye bei kwani kwa sasa asilimia 90 ya mwani inauzwa nje ikiwa ghafi na ni asilimia 10 tu ndio inayotumika hapa nchini.

Naye mkulima wa mwani, Mbimbisa Omary, alimshukuru Katibu Mkuu kwa kuwaletea vitendea kazi kwa ajili ya kilimo cha mwani.

Mbimbisa alisema kilimo cha mwani kinawasaidia mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuwasomesha watoto, kununua chakula pamoja na ujenzi wa nyumba.

Jaka Farahani, mkulima wa mwani, alisema changamoto ya masoko inawasumbua sana hasa pale wanunuzi wanaowategemea wasiponunua, hivyo aliiomba wizara kuwasaidia kutatua changamoto hiyo.

Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji (WMUV), Dk. Nazael Madalla, alisema wizara kupitia idara yake inaendelea kuhamasisha kampuni kuendelea kuchukua leseni kwa ajili ya kununua mwani na mpaka sasa zipo kampuni 7. Lengo la kuwa na kampuni nyingi ni kuongeza ushindani hivyo kampuni zinahamasishwa kujisajili ili zitambulike na ziweze kufanya biashara ya mwani.

# Maalim Seif: Kampeni zangu zimeenda vizuri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo jana, kilifunga kampeni zake katika viwanja vya Mnazi Mmoja Mjini Zanzibar, maelfu ya wananchi na wafuasi wa chama hicho walifurika viwanjani hapo.

Mgombea urais wa Zanzibar kupitia chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad, alisema kampeni zake zimeenda vizuri, hivyo endapo atakuwa rais, wananchi wategemee mambo mazuri ikiwamo kuboresha maisha yao.

Alieleza kuwa ataongeza mishahara ya watumishi wote na Zanzibar itanawiri.

"Nitaondoa uenevu, udhalilishaji na ukandamizaji," alisema Maalim Seif, ambaye ni mwenyekiti wa chama hicho.

Alieleza kuwa anashangaa Zanzibar kuendeshwa kijeshi, kila kona jeshi limetawala. Hata hivyo, hatutoa ufafanuzi wa kauli hiyo.

Maalim Seif alieleza kuwa hawatosusia uchaguzi mwaka huu, licha ya hujuma mbalimbali zinazofanywa dhidi yao.

Katika mkutano huo chama hicho kilipitisha bakuli la kuchangia chama, jumla ya shilingi milioni tatu zilipatikana viwanjani hapo kwa kutunisha mfuko kwa ajili ya uchaguzi.

Awali, hamasa na shauku, shangwe na nderemo za wafuasi hao ziliibuka wakati Naibu Katibu wa chama hicho Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, kuingia kiwanjani hapo majira ya saa 9:00 za jioni baada ya kuachiliwa akidaiwa kutekwa na watu wasiojulikana. Mazrui alidai kutekwa majira ya asubuhi eneo la Sateni Mjini Unguja wakati akielekea ofisini kwake Vuga.

Akizungumza katika mkutano huo, alisema siku ya jana ilikuwa ni ngumu sana kwake, lakini ameridhika kwa sababu ni ukombozi wa Wazanzibari.

"Nilipofika eneo la Sateni majira ya saa mbili ilikuja gari aina ya Prado ikatugonga na kupiga risasi juu na kuekewa bastola sita katika uso wangu na kubebwa, kufunikwa uso wote na kukabwa koo," alidai.

Alieleza kuwa saa saba mchana alitupwa katika pori la Bweleo na wale wanaosambaza kuwa hajatekwa ni waongo.

Alisema kila raia anahaki ya kushiriki katika siasa bila ya ubaguzi na ni haki ya kila mwananchi.

Akizungumza katika mkutano huo, Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho, Juma Duni Haji, aliendelea kusema msisitizo wao kuwa wataenda kupiga kura Oktoba 27 ambayo ni siku ya kupiga kura ya mapema ambayo hupiga watu maalum kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi.

Alisema wanataka kuleta mabadiliko ya utawala kwa sababu wameshateseka sana katika kutaka mabadiliko.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa kundi la kampuni za Barrick Gold, Mark Bristow (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya kampuni ya madini ya Twiga Mineral Corporation jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Twiga inaendeshwa kwa ushirikiano kati ya Barrick na Serikali ya Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mwinyi ahitimisha kampeni kwa kishindo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), jana, kimehitimisha kampeni zake za kuwanadi wagombea katika Viwanja vya Demokrasia, Kibanda Maiti, ambako kulifurika wananchi na wafuasi wa chama hicho waliokipamba kwa sare zao za rangi ya kijani na njano.

Mkutano huo uliohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali na chama hicho, akiwamo Rais mstaafu wa Awamu ya Nne wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Jakaya Kikwete, Rais wa Zanzibar mstaafu, Amani Abeid Karume, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein.

Mgombea wa urais wa Zanzibar kwa tiketi CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi Oktoba 28, kumpigia kura yeye na wagombea wote wa CCM, ili kuongoza Zanzibar, kuwaunganisha wananchi wote na kuleta maendeleo. Alisema tayari amejipanga kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar na kuzipatia ufumbuzi kero mbalimbali ambazo sasa anazifahamu kikamilifu.

Alisema amefanya mikutano 15 ya hadhara Unguja na Pemba pamoja na mikutano ya kuonana na makundi mbalimbali ya kijamii kwa kuwafuata walipo kwa ajili ya kusikiliza kero zinazowakabili ili akichaguliwa iwe rahisi katika kipindi kifupi na kuzifanyia kazi.

Alisema baada ya kuonana na makundi yote hayo yakiwamo ya wavuvi, wafanyabiashara ndogo pamoja na mamalishe, wakulima wa mwani na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi, Diaspora, sasa yupo tayari kuwatumikia.

"Baada ya kuonana na makundi na wananchi mbalimbali Unguja na Pemba na kusikiliza changamoto zinazowakabili...sasa napenda kusema rasmi kwamba dhamira yangu ipo tayari kuwatumikia wananchi wa Zanzibar na kuwaunganisha, kwa hivyo wananchi naomba kura ili ziniwezeshe niwe rais wa Zanzibar," alisema.

Aliahidi akichaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar, kisiwa cha Pemba kitapewa kipaumbele katika kuwavutia wawekezaji kuwekeza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa hoteli za kisasa zenye hadhi na viwanda vidogo katika eneo la maeneo huru ya uchumi.

"Kauli yangu ya kuzalisha ajira zipatazo 300,000 zitatokana na kuweka kipaumbele katika kisiwa cha Pemba kuwavutia wawekezaji kuwekeza katika miradi mbalimbali ikiwamo sekta ya utalii ni tunataka kuingiza zaidi ya watalii 800,000 kutoka 500,000," alisema.

Kwa upande wake Rais wa Zanzibar, Dk. Shein, alisema anamaliza muda wake wa miaka 10 ya urais akiwa ameshasaini sheria ya utafiti wa mafuta na gesi na rasilimali hiyo ni mali ya Zanzibar.

# Awamu ya tano yaipaisha Pwani kiviwanda

**Na Mwandishi Wetu,** PWANI

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ameeleza mafanikio ya mkoa huo ndani ya miaka mitano kuhamasisha ujenzi jumla ya viwanda 1,236 kulinganisha na mwaka 2015 ambapo kulikuwa na viwanda 300.

Ameeleza hayo wakati akifungua mkutano wa Baraza la Biashara la Mkoa linaloratibiwa na Baraza la Taifa la Biashara(TNBC) kujadili mafanikio na kuibua mapendekezo ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ndani ya mkoa na nchi kwa ujumla. "Kuna jumla ya viwanda vikubwa 68, viwanda vya kati 112, vidogo 168 na viwanda vidogo sana 888 jambo ambalo linadhihirisha mafanikio makubwa ndani ya mkoa katika kipindi cha uongozi wa awamu ya tano," alisema Ndikilo. Aliongezea mafanikio hayo yametokana na ushirikiano mzuri kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kuhakikisha malengo ya mkoa yanatekelezeka kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Mhandisi Ndikilo pia alielezea kuwa mkoa uliandaa maonyesho ya bidhaa kwa mwaka 2018/19 kwa lengo la kutambulisha bidhaa na kukuza soko la ndani na nje ya nchi jambo ambalo lilipokelewa vizuri na Watanzania wote. "Rai yangu kwa Watanzania ni kuwa wazalendo kwa kupenda kununua na kutumia bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi, jambo litakalosaidia kukuza ajira na pato la taifa kuongezeka," alisema.

Alisema mkoa umeweza kutengeneza ajira kwa zaidi ya 20% kwa mwaka 2020 ukilinganisha na 5% kwa mwaka 2015/16, ambapo zaidi ya Watanzania 200,000 wamepata ajira nchini. "Mafanikio haya yametokana na dhamira ya dhati ya Rais John Magufuli ya kutaka nchi kufikia uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025," alisema Ndikilo.

Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, alisema serikali imeboresha mazingira ya biashara na kupelekea idadi ya wawekezaji kuongezeka katika kipindi cha miaka mitano. "Uwekezaji wa nje umeongezeka kutoka Dola za Marekali milioni 850 mpaka kufikia Dola bilioni 1.1 jambo ambalo limeiongezea nchi fedha za kigeni na kufanya pato la taifa kuhimalika," alisema Dk.Wanga.

Aidha alieleza kuwa kupungua kwa riba za mikopo kwa mwaka kutoka asilimia 20 mpaka kufikia asilimia 14 na kuongezeka kwa mikopo benki na kufikia asilimia 7 inaonyesha namna ambavyo serikali imeendelea kuboresha mazingira na kufanya uchumi kukua. Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Mkoa wa Pwani, Jovita Mavoa, aliishukuru serikali kwa kutenga fungu ndani ya halmashauri iliwezesha kuwapatia elimu ya ujasiriamali na kuwafanya kufungua biashara zao na kuwafanya waweze kudumu maisha.

Masudi Ngingite mwenyeketi wa waendesha pikipiki Pwani, alisema waendesha shughuli zao kwa ufanisi kutokana na ushirikiano uliopo kati ya serikali na kundi hilo kwa kulifanya liendelee na shughuli za kuwaingizia kipato.

# Kilimo mpunga chawainua vijana

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATAFITI wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wamebaini kilimo biashara cha zao la mpunga kinacholimwa kwa wingi katika Bonde la Kilombero mkoani Morogoro, hivyo kuwainua kiuchumi vijana wa Wilaya ya Kilombero.

Prof. Ntengua Mdoe, alisema kupitia mradi wa Utafiti wa Sera za Kilimo Barani Afrika (APRA), wamebaini vijana wenye umri kati ya miaka 15-35 ambao ni sawa na asilimia 35.5 ya watu ndio wenye kunufaika zaidi katika bonde hilo.

Alisema hayo wakati akiwasilisha utafiti wake kwa waandishi wa habari wa kwenye warsha iliyoandaliwa na APRA.

Alisema pamoja na kuonyesha ushiriki wa vijana kwenye kilimo hicho, lakini bado wanakabiliwa na vikwazo ikiwamo ukosefu wa mitaji na mashamba ya uhakika ya kuendeshea kilimo hicho wengi wao wamekuwa wakikodi.

"Watafiti tumebaini kuwa sio kweli kwamba vijana hawashiriki kwenye shughuli za kilimo, bali wanashiriki vizuri kwenye kilimo cha mpunga na mpaka kwenye mnyororo wa thamani wa zao hilo katika maeneo mbalimbali," alisema Prof. Mdoe.

Alieleza kwenye utafiti huo umebaini vijana hao wamekuwa wakijipatia kipato kikubwa kinachotokana na kuwekeza katika kilimo hicho cha kufanyia shughuli za maendeleo kuliko nguvu inayowekezwa na vijana wanaofanya kazi zingine nchini.

"Kwenye utafiti wetu tumeshuhudia kuwa nyumba nyingi zinazoongozwa na vijana zina uhakika mkubwa wa chakula kuliko kaya ambazo zinaongozwa na wazee na watu wenye umri mkubwa, na hii ni kutokana na mafanikio makubwa wanayoyapata kutoka kwenye kilimo," alisema.

Hata hivyo, alisema katika mapendekezo ya utafiti huo wamezitaka halmashauri za wilaya na serikali kutenga ardhi ya kilimo kwa ajili ya vijana kama ambavyo imeelekezwa kwenye Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 ili kuwaondolea changamoto na kusaidia Taifa kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga.

Mapendekezo mengine ni kuwapo kwa njia sahihi ya kuwasaidia vijana hao mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya vijana pamoja na fedha zinazotolewa na halmashauri ya asilimia 10 kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ambapo vijana wametengewa asilimia nne. Naye Mkuu wa Mradi wa Utafiti wa Sera za Kilimo Barani Afrika upande wa Tanzania, Prof. Aida Isinika, alisema vijana wengi wanapenda kushiriki kwenye kilimo chenye tija na soko zaidi kama vile kilimo cha mpunga, vitunguu, nyanya na mazao mengine.


FSSP Field Support Services Project | Tanzania

**CONSULTANCY POSITION FOR FSSP EDUCATION TECHNICAL SPECIALIST**

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC) invites eligible candidates to indicate their interest to provide consultancy Services as an **Education Technical Specialist** to the Field Support Services Project (FSSP) Tanzania.

The **Education Technical Specialist** will provide technical support and advice to Global Affairs Canada in the development and implementation of a portfolio of projects and programs in the education sector. This includes, but is not limited to, advice in analysis, planning, management, monitoring and coordination of Canada's education programming and policy dialogue in Tanzania.

Candidates will be evaluated on the following key qualifications and experience:

i. A minimum of an undergraduate/Bachelor's degree from a recognized University;
ii. Fluency in spoken and written English. The ability to work in Kiswahili would be a strong asset;
iii. A minimum of five (5) years of cumulative, full-time, professional work experience in the education sector in Tanzania, in a non-teaching, non-clerical capacity (e.g. management, administration, advocacy, research, etc.);
iv. Experience in planning, designing, managing, monitoring and evaluating education projects and programs, using Results Based Management tools and processes, and drafting monitoring/evaluation plans and reports with recommendations; and
v. Experience in integrating cross cutting issues such as gender equality and environmental impact assessments;
vi. Demonstrated experience in providing advisory services in the following areas:
   - Primary education, non-formal education, teacher training, gender equality, or quality of education; and
   - Education sector reviews, donor coordination, or education sector technical and financial reporting.

In addition to the key qualifications above, the incumbent is also expected to demonstrate the following skills and competencies:

- Knowledge of education sector policy priorities and processes in Tanzania, including planning, management and budgeting of public sector resources;
- Excellent research, analytical and writing skills;
- Strong and demonstrated skills in leadership, teamwork, networking, coordination and intercultural communication;
- Previous experience in working with/ and or supporting a bilateral development agency; and
- Previous experience in working with the Ministry of Education, Science and Technology as an advisor, consultant, or technical specialist.

Interested candidates may obtain detailed description of these services by sending a request email to procurement@fssptz.org. Requests for further information will be received up to three working days prior to the submission deadline. Any request received later than that may not be responded to.

Interested candidates should send their Expressions of Interest (EoIs) ONLY electronically to procurement@fssptz.org not later than **06 November 2020** at **23:59 hours.** Late Expressions of Interest shall not be accepted for evaluation, irrespective of the circumstances.

**FSSP Manager**

215959102



**SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA (TPDC)**

**SHINDANO LA UTENGENEZAJI WA NEMBO/LOGO YA TPDC/ SHIRIKA LA MAFUTA LA TAIFA**

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ni Shirika la serikali lililoanzishwa mwaka 1969 kupitia tangazo la Serikali Na. 140 la tarehe 30 Mei 1969 chini ya sheria ya mashirika ya umma namba 17 ya mwaka 1969. Sheria ya mafuta ya mwaka 2015 (PA, 2015) iliibadilisha hadhi TPDC kuwa Shirika la Mafuta la Taifa (National Oil Company-NOC) chini ya Wizara ya Nishati, likiwa na jukumu kubwa la kufanya utafutaji, uzalishaji, uendelezaji na usambazaji wa wa nishati ya mafuta na gesi asilia hapa nchini.

Katika kutekeleza majukumu yake, TPDC imeanzisha kampuni tanzu mbili, Kampuni ya kwanza inajulikana kwa jina la TANOIL inayojihusisha na biashara ya usambazaji wa mafuta ya petroli pamoja na bidhaa zake, na kampuni ya pili inajulikana kwa jina la GASCO ambayo ina jukumu la kusimamia uendeshaji na usimamizi wa miundombinu ya gesi asilia.

Kutokana na mabadiliko haya shirika limeanzisha mchakato wa kubadilisha chapa na taswira yake na tunapenda kuutangazia umma kuhusu shindano la ubunifu wa kutengeneza nembo/logo mpya ya taasisi..
Lengo la shindano hili la ubunifu wa kutengeneza nembo/logo ya shirika ni kutoa fursa kwa wachoraji na wabunifu wa Tanzania kupendekeza nembo/logo ya shirika kwa niaba ya wananchi wa Tanzania.

Shindano hili litawahusisha na kuwashindanisha wabunifu na wachoraji wanaochipukia, wabobezi, na wanafunzi wa shule za msingi, sekondari, na vyuo nchini.

**Utaratibu wa namna ya kushiriki**
Wachoraji na wabunifu wote ambao wangependa kushiriki katika shindano hili watume michoro yao katika mfumo wa PDF, majina kamili, na namba ya simu kupitia barua pepe yenye somo **"Shindano la Nembo TPDC"** kwenda **pr@tpdc.co.tz** kabla ya tarehe 6 Novemba 2020 saa 11 kamili jioni.

**Tangazo la Washindi**
Washindi wa shindano hili watatangazwa na shirika kupitia vyombo vya habari siku ya Alhamisi tarehe 12 Novemba 2020 na zawadi kwa washindi watatu kukabidhiwa tarehe 18 Novemba 2020, Dodoma, Tanzania.

**Zawadi**
Zawadi nono zitataolewa kwa mshindi wa kwanza hadi wa tatu

**Mawasiliano: Iandikwe Juu ya bahasha : Shindano la Nembo TPDC**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**S.L.P 2774**
**Dar es salaamu**
**Au wasiliana nasi kwa simu namba:**
**+255 22 2200103/4 au 22000112**
**0766268427; 0682157530**

**Imetolewa na :**
**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano,**
**TPDC**
**#tpdctunawezesha**

215959402

# RC aonya vijana kufanya fujo Jumatano

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, ameawaonya vijana mkoani humo kuacha kurubuniwa na baadhi ya wanasiasa kujipanga kufanya fujo siku ya uchaguzi mkuu Oktoba 28, mwaka huu, wa kuchagua madiwani, wabunge, na Rais.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Shinyanga, ikiwa zimebaki siku mbili kufanyike uchaguzi mkuu.

Alisema kumekuwapo na tetesi juu ya vijana kutaka kufanya fujo siku ya uchaguzi mkuu, na kuwataka waache, ikiwa serikali imejipanga vyema kudhibiti aina yoyote ile ya viashiria vya uvunjifu wa amani.

"Tarehe 28 mwezi huu ambayo ni siku ya Jumatano, tutakuwa na uchaguzi mkuu, hivyo nitoe tahadhari kwa vijana wasirubunike kufanya fujo zozote zile, bali tutawashughulikia, tunataka uchaguzi umalizike kwa amani," alisema Telack.

"Amani hii tuliyonayo hapa nchini, mataifa mengi yanatamani ivurugike, na sisi hatutakubali, mtu ukishindwa kubali matokeo, uchaguzi ni kama mpira, ukifungwa goli jipange mchezo ujao," aliongeza.

Pia alisema wameshatoa maelekezo kwa wasimamizi wa uchaguzi, kuwa watu wenye mahitaji maalumu wakiwamo wazee, wajawazito, na wenye watoto wadogo, wapewe kipaumbele kuanza kupiga kura na siyo kujipanga mstari. Katika hatua nyingine Telack, amewaonya waandishi wa habari, wasitangaze matokeo kwenye vituo vya kupigia kura, bali kazi hiyo ni ya msimamizi wa uchaguzi wa jimbo husika, ili wasije wakaleta taharuki.




Kaimu Ofisa Mkuu Kitengo cha Biashara wa Tigo Tanzania, David Umoh, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) katika uzinduzi wa kampeni ya siku 90 inayojulikana kama 'Jaza Tukujaze Tena', ambayo lengo lake ni kuwafanya wateja kuwa washindi wa zawadi mbalimbali kila wanaponunua bando za siku, wiki au mwezi. Wengine ni Mkuu wa Idara ya Masoko wa Tigo, William Mpinga (kulia) na Balozi wa kampeni hiyo, Lucas Lazaro Mhuvile maarufu Joti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kagera, Iringa zapewa vifaa vya afya

**Na Mwandishi Wetu**

MIKOA ya Iringa na Kagera imepigwa jeki kwa kupatiwa vifaa mbalimbali vya afya vyenye thamani ya Sh. milioni tisa.

Mikoa hiyo imenufaika kwa uwezeshaji huo kutoka Benki ya NMB ikiwa ni sehemu ya kurudusha faida kwa jamii.

Mbali na vifaa hivyo benki hiyo kupitia kwa wafanyakazi wake katika mkoa wa Iringa wametoa zawadi za vifaa vya shule kwa wanafunzi wa shule tatu za msingi zilizoko katika Manispaa ya Iringa pamoja na kuwapa wanafunzi hao elimu ya kifedha kwa manufaa yao baadaye maishani.

Shule zilizotembelewa na benki hiyo ni ya Msingi Mapinduzi, Shule ya Msingi Wilolesi na Shule ya Msingi Saint Dominic ambapo wafanyakazi wa NMB walikwakabidhi zawadi hizo ikiwa ni moja ya kuadhimisha wiki ya wateja wa benki hiyo.

Katika Mkoa wa Iringa benki hiyo, imetoa vifaa kwenye Hospitali ya Rufani ya mkoa huo ambapo vifaa vilivyotolewa ni mashuka, vitanda vya kujifungulia kwa kinamama, na vitu mbalimbali kwa ajili ya watoto.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa mgamga mkuu wa mkoa huo, Dk. Robert Salim, Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja wa NMB, Abella Tarimo, alisema:

"Tunatambua kwamba baadhi ya sekta zinakabiliwa na changamoto ikiwamo sekta ya afya hivyo kama NMB inatambua kwamba kinamama wanajifungua na hawana vifaa vya kujifungulia hivyo nafasi hii tumetumia kuleta vifaa hivyo kwa Hospitali ya Rufani ya Iringa."

Alisema kuwa licha ya mashuka pia wamekabidhi hospitali hapo pampasi za watoto, mafuta ya kujipaka, sabuni, rubber shit zinazotumika kwa ajili ya kuweka chini ya mashuka kwa kinamama wakati wa kujifungua.

Akipokea msaada huo Mganga Mkuu wa Mkoa alishukuru kwa msaada huo akieleza kuwa umefika wakati mwafaka kwani kumekuwa na upungufu wa baadhi ya vifaa kulingana na idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa hospitalini hapo kutoka ndani na nje ya mkoa.

Katika Mkoa wa Kagera benki hiyo imekabidhi vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni tano katika Kituo cha Afya Rubale Wilaya ya Bukoba Vijijini, ambapo vifaa hivyo vilivyotolewa ni vitanda sita na magodoro yake na mashuka.

Akikabidhi vifaa hivyo Meneja wa Benki hiyo Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus, alisema NMB imechangia vifaa vya shilingi milioni 25 tangu mwezi Januari mwaka huu kwa ajili ya kuboresha huduma za afya mkoani Kagera kama sehemu ya jitihada za benki hiyo kuunga mkono hatua za serikali za kuboresha sekta hiyo nchini.

Akipokea vifaa hivyo, Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Bandiati Gangole, alisema kuwa msaada huo utapunguza adha iliyowapata wagonjwa waliofika kupata huduma katika kituo hicho ikiwa ni pamoja na sehemu ya wajawazito kujifungua ambayo kabla ya msaada huo haikuwa na kitanda chochote.

## Ufuatiliaji kahawa kumpaisha mkulima

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

UFUATILIAJI na usimamizi wa kilimo bora katika zao la kahawa utasaidia kunufaisha mkulima na kupata mafanikio ya tani 200,000 zitakazofikia asilimia 5 ya malengo ya soko la dunia.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Kahawa, Prof. Jamal Adamu, kwenye uzinduzi wa ugawaji miche ya kahawa kwa baadhi ya wakulima kutoka wilaya za Mkoa wa Kagera iliyozalishwa katika kitalu cha Gereza la Kitengule wilayani Karagwe na JJAD Kagera Farmers (T)LTD wilayani Kyerwa, lengo likiwa ni kusaidia mkulima kuongeza uzalishaji na kupata kipato.

Adamu alisema Bodi ya Kahawa kwa ushirikiano na kampuni ya JJAD Kagera Farmers, Cafe Africa inatenga miche milioni 20 kila mwaka kwa ajili ya kugawa kwa mkulima kama sehemu ya kujiongezea uzalishaji na kuendeleza kuingia katika masoko ya dunia.

"Bodi inaamini kuanzisha vitalu hivi viwili hapa mkoani ni malengo ya ongezeko la uzalishaji wa kahawa ya maganda, kwani mategemeo yaliyopo ni kufikia kuzalisha miche milioni 20 kwa mwaka ambayo itarahisisha Taifa kuwa na uongezaji wa tani 200,000 za kahawa," alisema Prof. Adamu.

Katibu Tawala mkoani Kagera, Prof. Faustine Kamuzora, alisema, kuanzisha mradi wa miche uendane na aina tatu za wakulima na kuona hali ya uwezo wa kununua na kwamba malengo ya pamoja ni kuona mkulima anapata kipato.

"Niseme tu miradi hii inayomlenga mkulima iangalie hata wale wa hali ya chini, kiwango cha kati na juu kwa sababu ujio wa miche hiyo umetokana na pesa inayotoka katika pato la wakulima wa aina zote na sio walio na hali ya juu," alisema Prof. Kamuzora.

## Mgombea aahidi kuwasomesha watakaofaulu vizuri kidato cha 4

**Na Happy Severine,** BARIADI

MGOMBEA ubunge Jimbo la Bariadi mkoani Simiyu kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mhandisi Andrea Kundo, ameahidi kuwasomesha wanafunzi wa kidato cha nne ambao watapata ufaulu wa daraja la kwanza alama saba na nane katika mtihani wa kitaifa mwaka huu.

Kundo alisema kuwa mwanafunzi mbaye atapata ufaulu huo, atamsomesha kidato cha tano na sita hadi chuo kikuu na gharama zote za masomo zitakuwa juu yake.

Mgombea huyo alitoa ahadi hiyo wakati wa kampeni zake katika Kata ya Ngulyati, mbele za wanafunzi wa shule ya sekondari inayomilikiwa na Kanisa la Wasabato iliyoko kwenye kata hiyo. "Mwanafunzi yeyote wawe wengi au mmoja, ambaye atapata ufaulu wa daraja la kwanza alama 7 na 8, gharama za kuendelea hadi chuo kikuu, zitakuwa juu yangu," alisema Mhandisi Kundo. Aidha, alisema kuwa endapo atachaguliwa atahakikisha anaboresha sekta ya elimu katika wilaya hiyo, ikiwamo kuboresha miundombinu yake ili kuwa rafiki kwa wanafunzi na walimu.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara na wananchi wa kata hiyo, Kundo aliahidi kutengeneza barabara kutoka kwenye kata hiyo hadi makao makuu ya wilaya kupitia Kijiji cha Ditima. "Kwa muda mrefu wananchi wa huku wamekuwa wakiteseka kwenda makao makuu ya halmashauri, wanalazimika kupitia Bariadi Mjini, kutokana na barabara hii kutopitika, nichagueni mimi itapitika muda wote," aliahidi Kundo.

Nipashe
Spotika




AZAM INAVYOCHAPA MCHANA, JIONI, USIKU UK. 14




# SAJILI 5-BORA ZA 'USIKU' ARSENAL

## ISIKUPITE

AJAX imekuwa timu ya kwanza Ligi Kuu Uholanzi 'Eredivise', kufunga mabao 13 katika mchezo mmoja baada ya Jumamosi kuibuka na ushindi wa mabao 13-0 dhidi ya VVV-Venlo. Kikosi hicho cha Kocha Erik ten Hag (pichani), kimevunja rekodi yake ya mwaka 1972 kilipoifunga Vitesse 12-1 katika ligi hiyo.



**LONDON,** England

KWA usajili wa Thomas Partey, Arsenal kwa mara nyingi tena ilifanikiwa kumpata mtu waliyemhitaji kwa muda mrefu, lakini katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa pazia la usajili.

Kwa miaka mingi wachezaji wengi wametua pale kwenye dimba la Emirates katika siku ya mwisho ya usajili na mara nyingine usiku wa manane kabla ya dirisha kufungwa.

Hapa tunaangalia sajili tano bora za Arsenal za siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili, haya sasa...

### #5. NACHO MONREAL - MALAGA KWENDA ARSENAL, 2013

Baada ya kuumia kwa Kieran Gibbs, ambaye alikuwa chaguo la kwanza la Arsenal kama beki wa kushoto kutokana na kuondoka kwa Gael Clichy aliyehamia Manchester City, 'Washikabunduki' hao hawakuwa na chaguo jingine zaidi ya kuingia sokoni.

Zikiwa zimebakia saa kadhaa za kufungwa kwa pazia la usajili Arsene Wenger akaingia sokoni na kumsajili Nacho Monreal kutoka Malaga kwa pauni milioni tisa.

Monreal alitumia misimu nane hapo London akicheza mechi 251 na kufunga mabao 10. Akacheza fainali mbili za Ligi ya Europa na kushinda mara mbili Kombe la FA.

### #4. MIKAEL ARTETA - EVERTON KWENDA ARSENAL, 2011

Ulikuwa ni msimu mbaya wa mwaka 2011, wakati Arsenal walipompoteza Gael Clichy, Samir Nasir na Cesc Fabregas. Hivyo walihitaji kuimarisha kikosi chao.

Siku mbili kabla yakufungwa kwa pazia la usajili, Arsenal wakamsajili Mikel Arteta ambaye alikuwa amejiimarisha yeye mwenyewe kule Everton.

Arteta alikuwa kule Everton kwa misimu nane na pengine ndiye mchezaji wao bora zaidi na alitua pale kweye dimba la Emirates kwa ada ya pauni milioni 10.

Arteta akawa nahodha aliyeiongoza Arsenal kwenye fainali ya Kombe la FA mwaka 2014 na kulibea taji lao la kwanza kwa kipindi cha miaka nane.

Akiwa Arsenal alicheza mechi 150 na kufunga mabao 16 na alikuwa nahodha katika misimu yake miwili ya mwisho.

### #3. PIERRE EMERICK AUBAMEYANG - BORUSSIA DORTMUND KWENDA ARSENAL, 2018

Ulikuwa tena msimu mwingine ambako Arsenal ilipoteza nyota wake kadhaa. Alexis Sanchez alihamia Manchester United kwa kupishana na Henrikh Mkhitaryan.

Pierre Emerick Aubameyang akafanywa kuwa mbadala wake katika usajili wa Januari ambao ulikuwa ghali zaidi katika historia ya Arsenal.

Arsenal ilitumia kiasi cha pauni milioni 56 ili kumsajili Aubameyang wakati huo wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Usajili wa Aubameyang umekuwa na mafanikio kwa Arsenal kwani kwa sasa ndiye nahodha wake. Kwa sasa akiwa na miaka miwili na nusu klabuni hapo, amefunga mabao 72 katika mechi 114 alizocheza hapo.

### #2. PER MERTESACKER - WERDER BREMEN KWENDA ARSENAL, 2011

Mertesacker ni mchezaji mwingine aliyetua Arsenal wakati wa kufungwa kwa pazia la usajili mwaka 2011 hasa baada ya 'Washikabunduki' hao kukabiliwa na majeruhi na hiyo ni baada ya kuchezea kichapo cha mabao 8-2 kutoka kwa Manchester United.

Wenger akaingia sokoni na ili kuimarisha safu yake ya ulinzi kwa kumsajili Per Mertesacker kutoka Werder Bremen kwa ada ya pauni milioni nane.

Raia huyo wa Ujerumani alicheza mechi 221 huku pia akiwa nahodha wa kikosi hicho.

### #1. MESUT OZIL - REAL MADRID KWENDA ARSENAL, 2010

Ozil ndio ulikuwa moja ya usajili wa Arsenal wa kushitua zaidi.

Raia huyo Ujerumani alikuwa ndiye kwanza kamaliza msimu akiwa nyota bora wa pasi za mwisho akiwa na 29. Kila mmoja na mchezaji mwenyewe, alitarajia kwamba Real Madrid wangembakiza kiungo huyo.

Na alicheza mechi mbili za ligi kwa 'Los Blancos' kabla ya hali kubadilika haraka. Ozil akawekwa sokoni na Arsenal walimsajili kwa pauni milioni 42.5 - ambapo ilikuwa ada kubwa zaidi kwa kipindi hicho. Licha ya nyota kadhaa wa Real Madrid kupaza sauti asiuzwe, Madrid wakamuuza.

Ozil akaja kuwa mhezaji bora na muhimu zaidi kwa Arsenal na chini ya Wenger alitengeneza pasi za mwisho zaidi 70 katika mashindano yote kwa kipindi cha misimu mitano ya kwanza.

Lakini baada ya kuondoka kwa Wenger mambo yakawa magumu sana kwa Ozil.

Na sasa Ozil hayupo kwenye kikosi cha kocha Mikel Arteta. Amecheza mechi 254 na kufunga mabao 44 tangu alipojiunga na timu hiyo mwaka 2013.



# AZAM INAVYOCHAPA MCHANA, JIONI, USIKU

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kesho ikitarajiwa kucheza mechi yake ya raundi ya nane dhidi ya Mtibwa Sugar, timu ya Azam FC ndiyo timu pekee Tanzania ambayo imeshinda mechi zake kwenye majira tofauti.

Azam ambayo imevunja rekodi yake iliyoweka kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2015/16 kwa kushinda mechi saba mfululizo, imeshinda mechi zake mchana, jioni na usiku, huku kukiwa si tu kwamba hakuna timu iliyoshinda mechi saba mfululizo kwenye mechi za ligi, lakini kushinda kwenye majira tofauti.

**Kocha msaidizi wa timu hiyo, Vivier Bahati alisema kuwa ushindi huo wa saba mfululizo ni dalili za kuwa msimu huu wamedhamiria kuusaka ubingwa na ndiyo maana wanajitahidi sana kushinda mechi za ugenini.**

"Lengo letu msimu huu ni ubingwa na inavyoonekana ni kwamba huwezi kuwa bingwa bila kushinda mechi za ugenini na nyumbani, ndiyo maana unaona tunakazana kupata ushindi ugenini, lakini pia nyumbani," alisema kocha huyo.

Azam ambayo ilitwaa ubingwa msimu wa 2013/14, rekodi yao safi ilikuwa ni kushinda mechi tano mfululizo kabla ya kutoka sare mechi ya sita msimu wa 2015/16 ambao Yanga ndiyo ilitwaa ubingwa.

Msimu wa 2015/16 Azam ilianza ligi kwa kuichapa Prisons mabao 2-1, ikaiadhibu Stand United kwa mabao 2-0. kabla ya kuichapa Mwadui FC bao 1-0 na kuifunga Mbeya City 2-1, halafu ikaishindilia Coastal Union 2-0.

Baada ya kushinda mechi tano mfululizo, Azam ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga na rekodi yao ya kushinda mechi mfulululizo ikaishia hapo.

Msimu huu Azam imeshinda mechi saba mfululizo kwenye majira tofauti na zifuatazo ndiyo mechi ilizocheza na muda wake...

**Mechi za mchana**
**AZAM 1-0 MBEYA CITY**

Hii ni mechi ya kwanza kwa Azam kucheza majira ya saa nane mchana. Ilicheza ugenini kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya na kutoka mbabe kwa bao 1-0. Lilikuwa ni bao la dakika ya 24, lililofungwa na Ally Niyonzima, mechi ikichezwa Septemba 20, mwaka huu.

**AZAM 2-0 IHEFU FC**

Oktoba 20, Azam ilicheza mechi yake nyingine saa nane mchana wa jua kali ikiwa ugenini kwenye Uwanja ule ule wa Sokoine mjini Mbeya. Safari hii ikicheza dhidi ya Ihefu FC na kushinda mabao 2-0. Yalikuwa na mabao ya Ayoub Lyanga dakika ya 54 na Idd Nado dakika ya 83 yakiifanya timu hiyo kushinda mechi zake zote mbili ilizocheza mchana mpaka sasa.

**Mechi ya jioni**
**AZAM 1-0 PRISONS**

Mpaka sasa Azam imecheza mechi moja tu ya jioni ya kuanzia saa 10:00 jioni, ikichezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga dhidi ya Prisons. Kwenye mechi hiyo Azam ilishinda bao 1-0 lililofungwa na Prince Dube dakika ya 89.

**Mechi za usiku**
**AZAM 1-0 POLISI TANZANIA**

Azam ambayo ikicheza kwenye Uwanja wa Azam Complex hucheza kuanzia saa moja usiku, ilianza kucheza mechi zake Septemba 7, mwaka huu, ikicheza dhidi ya Polisi Tanzania na kushinda bao 1-0. Bao hilo lilifungwa dakika ya 44 na Obrey Chirwa.

**AZAM 2-0 COASTAL UNION**

Septemba 11, mwaka huu, Azam ilicheza mechi nyingine usiku kwenye uwanja wao wa nyumbani dhidi ya Coastal Union na kushinda mabao 2-0. Yalikuwa ni mabao ya Mzimbabwe anayeongoza kwenye utupiaji Ligi Kuu mpaka sasa, Prince Dube aliyefunga yote mawili kwenye dakika ya 68 na 88.

**AZAM 4-2 KAGERA SUGAR**


Azam ilipata ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Kagera ikicheza usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex Oktoba 4, mwaka huu. Dube alifunga mabao mawili dakika ya tano na 87, Chirwa akifunga moja dakika ya 47 na Richard Djodi akiipatia bao la nne dakika ya 51.

Mabao ya Kagera Sugar yalifungwa na David Luhende dakika ya 33 na Yusuph Mhilu dakika ya 50.

**AZAM 3-0 MWADUI FC**

Ikiwa kama vile imeufanya uwanja wake wa nyumbani kuwa machinjio, Azam iliandikisha ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mwadui FC Oktoba 15, mwaka huu. Chirwa alifunga mabao mawili, dakika ya 27 na 62, huku Dube akifunga bao moja dakika ya 60.

**JE, WAJUA?**



EDOUARD Mendy amekuwa kipa wa kwanza Chelsea kuweza kumaliza mechi bila kuruhusu bao [clean sheet] katika mechi zake mbili za kwanza za Ligi Kuu kwa klabu hiyo tangu Petr Cech alipofanya hivyo Agosti 2004. Lakini amekuwa kipa wa kwanza Chelsea kumaliza na 'clean sheet' katika mechi za Ligi Kuu kwenye Uwanja wa Old Trafford tangu Thibaut Courtois alipofanya hivyo Desemba 2015.



# Viongozi dini wakumbushwa kuhubiri amani uchaguzi mkuu

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

ZIKIWA zimesalia siku mbili kuelekea Oktoba 28, siku ya kupiga kura nchini, Kamati ya Amani ya Mkoa wa Dodoma, imewataka viongozi wa dini kuhubiri amani na kuhamasisha waumini wao kujitokeze kwa wingi ili kutimiza haki yao ya msingi ya kupiga kura.

Kamati hiyo inaundwa na viongozi wa dini kutoka madhehebu mbalimbali ya mkoa huo.

Katika kikao chao na Kamati ya Ulinzi na Usalama mkoani humo jana, wajumbe wa kamati hiyo walionesha kutofurahishwa na baadhi ya viongozi wanaohamasisha waumini wao kutopiga kura kwa madai kuwa jambo hilo ni haramu.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Mwenyekiti wa Kamati ya Amani mkoani humo, Shekhe Rajab Shaban, alisema kupiga kura sio haramu na kutaka kupuuza maneno hayo.

Naye, Askofu Mkuu wa Kanisa la Philadephia Gospel Assembly Dodoma, Dk. Yohana Masinga, aliwataka viongozi wa dini kulinda vinywa vyao kwa kuwa vinaweza kuharibu amani badala ya kuhamasisha watu na kutaka amani itunzwe.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema kuna mataifa kwa sasa wananchi wake wanahangaika kutokana na amani kuvurugwa kwa zaidi ya miaka mitano.

"Kuna nchi tangu amani imevurugika hakuna maendeleo yanayofanyika, miaka mitano wananchi wanahangaika hakujatulia, wale waliokuwa na malengo yao unakuta walishakimbia siku nyingi," alisema.

Kadhalika, Katibu Tawala wa Mkoa huo, Maduka Kessy, alisema ni vyema viongozi wa dini wakaweka pembeni ushabiki wa vyama na kutimiza wajibu wao wa kuhakikisha wanahamasisha waumini wao kulinda amani.

Katika hatua nyingine, Kanisa la Uweza wa Bwana Tanzania, jijini Dodoma, limefanya maombi maalum ya kuombea Taifa kufanya uchaguzi kwa amani.

Akizungumzia maombi hayo, Katibu Mkuu wa Kanisa hilo, Boniface Kisinga, alitoa rai kwa Watanzania kutokubali kushawishiwa au kuonesha viashiria vya uvunjifu wa amani na kuwakataa watu ambao hawaoni maana ya amani iliyopo.



Mwenyekiti wa kikundi cha kuzalisha kuku na ufugaji cha Tusumuke, Christopher Dioniz (kushoto), akimpa maelezo Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge (wapili kushoto) alipotembelea banda hilo kwenye maonyesho ya wajasiriamali yaliyofanyika jana, viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waomba katazo kuchimba mchanga eneo la zabibu

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limeombwa kuweka katazo la uchimbaji mchanga kwenye eneo la kilimo cha zabibu, nyanya na mboga lililopo Kata ya Matumburu jijini Dodoma kutokana na kuwapo uharibifu wa mazingira.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Chama cha Tupendane Group kinachojishughulisha na kilimo hicho, Donald Masebo, alisema kumekuwapo na uharibifu unaofanywa na wachimba mchanga kwenye mkondo wa maji wanayotumia kumwagiliaji mazao yao.

Masebo alisema kwa muda mrefu wananchi hao wamekuwa wakitumia eneo hilo kujipatia fedha, lakini uchimbaji huo unaathiri kilimo hicho.

"Kwa kweli sisi wanakikundi tunalazimika kuomba NEMC waje waweke katazo kuhusu eneo hili ambalo hata serikali ya mtaa na kata inaonyesha kwa kiasi kikubwa imeruhusu kumweka mwekezaji kuchimba mchanga na kuharibu mazingira yake," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema licha ya serikali ya mtaa kumruhusu mwekezaji huyo, lakini hawajawahi kukaa na wakulima na mwekezaji huyo ili kuangalia namna ya kunufaika na eneo lao kutokana na kutoendesha shughuli za kilimo kwa sasa.

Kwa upande wake, mwekezaji aliyepewa eneo hilo kuchimba mchanga, Onesmo Chigoma, alisema anafanya shughuli hiyo kihalali na ana vibali vya kuruhusu kuchimba mchanga. "Mimi siwezi kuvamia maeneo ya kuchimba mchanga bila kupitia serikali husika kwa ajili ya kupatiwa kibali cha kuniruhusu, hata hivyo ninashangaa kuona kikundi cha Tupendane Group kilichokuwa kinalima kwenye eneo hilo kutaka kunizuia wakati vikao mbalimbali vilishafanyika na mimi kuniruhusu kisheria," alisema.

Akizungumzia suala hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Ukombozi, Haruna Nyakapala, alisema kuwa mwekezaji huyo anafanya shughuli hiyo kwa mujibu wa sheria.

Alisema kuwa kibali amepewa baada ya maofisa mazingira kufika kwenye eneo hilo la korongo na kudai kwamba halina shida yoyote kufanya shughuli za uchimbaji.

Hata hivyo, alisema kuwa mwekezaji huyo anayechimba mchanga aliruhusiwa kuchimba baada ya kukaa kwa pamoja na kikundi hicho na kuridhia.

## SUMA JKT yaokoa mil. 400/- kiwandani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), limeokoa Sh. milioni 400 katika ujenzi wa kiwanda cha mabati na misumari jijini Dodoma, kwa kutumia nguvu kazi yao wakiwamo vijana na maofisa wa kujitolea.

Akizungumza baada ya kukagua ujenzi wa kiwanda hicho, Kaimu Mkuu wa Tawi la Utawala JKT, Kanali Hassan Mabena, alisema hadi kukamilika kwake kiwanda hicho kitagharimu Sh. bilioni 1.7 na Sh. milioni 400 zitaokolewa kwenye ujenzi huo ambao kwa sasa umefikia asilimia 85.

Kanali Mabena alisema kinatarajiwa kiwanda kuanza kufanya kazi mwakani.

"Majengo ya serikali na watu binafsi yamekuwa yakijengwa kwa kasi kubwa, hivyo kasi ya miundombinu kutokana na serikali kuhamia Dodoma, imekuwa kubwa na uhitaji wa mabati na misumari ni kubwa na kushindwa kutosheleza soko la Dodoma, hivyo JKT wakaamua kuanzisha kiwanda hiki," alisema.

Aidha, alisema kiwanda kitasaidia kuwanufaisha wakazi wa Dodoma ikiwamo kutoa ajira kwa vijana.

Alieleza kuwa JKT imekuwa ikitoa gawio kwa serikali, hivyo kiwanda hicho kitachangia kuongeza pato la taifa, lakini pia kuongeza gawio kwa serikali.

Kadhalika, alisema jeshi hilo lina mpango wa kuanzisha viwanda vingine vya mazao ya kilimo mifugo na uvuvi, ambapo tayari kuna kiwanda cha kuchakata mahindi cha mlale Songea na mpunga kilichopo Chita Ifakara.

"Uchumi wa nchi umekuwa na kufikia uchumi wa kati kama jeshi tunalo jukumu la kuhakikisha tunaunga jitihada za serikali ili kufikia uchumi wa juu zaidi," alisema Kanali Mabena.

Kanali Mabena aliwataka vijana wanaojenga kuzingatia maelekezo ya ujenzi ili mkataba ukiisha waende wakafanye kazi hizo mitaani.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mradi wa kiwanda hicho, Meja Erasto Tesha, alisema katika utekelezaji wa mradi huo tayari wamepokea Sh. milioni 457.3 ambapo kiasi cha Sh. milioni 420.4 zimeshatumika.

Meja Tesha alisema wanawashukuru vijana wanaojitolea katika ujenzi kwa kufanya kazi kwa weledi mkubwa kwenye mradi huo.

"Tunawashukuru sana vijana wanaojenga kwa sababu wanafanya kazi iliotukuka hivyo wanastaili sifa, natoa rai kwao kuwa makini na kazi wanazofanya maana zitawasaidia hapo mbeleni," alisema.





# Polisi yadai kuna njama kuvuruga uchaguzi mkuu

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limesema limepata taarifa kuwa kuna baadhi ya vyama vya siasa vimewakodisha wahalifu kutoka kwenye mikoa mbalimbali nchini kwa ajili ya kuvuruga uchaguzi kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, aliyasema hayo juzi wilayani Mbarali alipokuwa anakabidhiwa Kituo cha Polisi kilichojengwa na Kampuni ya Mbarali Estate.

Matei alisema jeshi hilo linaendelea kufuatilia taarifa za watu hao, ili kujua walipohifadhiwa ili wadhibitiwe mapema kabla ya siku ya uchaguzi haijafika.

Aliwataka wananchi wa wilaya zote za mkoa huo kutoa taarifa kwa jeshi hilo hasa wanapobaini kikundi chochote cha watu ambao hawawafahamu ili wachunguzwe mapema kabla hawajaleta matatizo kwenye maeneo yao.

"Siku ya uchaguzi wananchi wote mnahamasishwa kujitokeza kwenye vituo vyenu vya kupigia kura, sisi tumejiandaa kwa ajili ya kuhakikisha amani na utulivu vinatamalaki ndani ya maeneo yote ya mkoa wetu, endapo utamuona mtu anayehatarisha amani toa taarifa mapema," alisema Matei.

Alisema mkoa huo sio mkoa wa kufanyia majaribio na hivyo akawataka wahalifu hao waliokodiwa kutoka kenye mikoa mingine kuondoka mapema kabla hawajanaswa na kutiwa nguvuni.

Alisema kila Mtanzania ana wajibu wa kulinda amani iliyopo kwa sasa na hivyo akawataka wananchi wote kushiriki kuilinda badala ya kuliachia Jeshi la Polisi pekee.

# Kinamama waeleza barabara ilivyowaathiri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wanawake wa Kata ya Kalobe jijini Mbeya, wamedai kuwa wamekuwa wakipata matatizo ya uzazi kutokana na ubovu wa barabara inayounganisha kata hiyo na barabara kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM).

Walitoa kauli hiyo juzi wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ilipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 6.5 kwa kiwango cha lami, ambapo walisema ndoa zao zilikuwa matatani.

Elizabeth Kibona, alisema barabara hiyo ilikuwa imejaa mashimo, hivyo usafiri pekee ambao walikuwa wanautumia ni pikipiki za abiria maarufu kwa jina la bodaboda na bajaji.

Alisema kutokana na mashimo ya barabara hiyo, wanawake wengi mimba zilikuwa zinatoka wanaposafiri hasa kwa kurushwarushwa na vyombo hivyo kwenye makorongo hali ambayo ilikuwa inasababisha mizozo kwenye familia.

"Ndoa zetu zilikuwa na migogoro mingi kwa sababu ya hii barabara yetu, kusafiri kutoka hapa mpaka njia panda ya Itende ilikuwa ni kazi kubwa sana, tulikuwa tunarushwa kwenye mashimo mpaka mimba zinatoka, lakini wanaume walikuwa wanaamini kuwa sisi wake zao tuna matatizo kitu ambacho sio kweli," alisema Elizabeth.

Aliishukuru serikali kwa kuamua kuijenga barabara hiyo kipindi hiki cha kuelekea masika akidai kuwa ndicho kilichokuwa kinakuwa kipindi kigumu zaidi kwao. Naye Subilagha Mwakasungura, alisema walikuwa wanapata ajali mara kwa mara kwenye barabara hiyo kwa kuanguka na pikipiki ama bajaji kutokana na ubovu wa barabara na kwamba walikuwa wamekata tamaa kuwa wamesahaulika. Alisema kwenye bajaji hizo kulikuwa kunajaa kelele wanaposafiri kwa sababu zilikuwa zikiyumba watu wanaamini kuwa zinataka kuanguka, lakini kwa sasa baada ya kuanza kutengenezwa hali imeanza kuwa shwari. Akitoa taarifa ya ujenzi wa barabara hiyo, Mratibu wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wa Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Gerald Matindi, alisema barabara hiyo wanaijengwa kwa gharama ya Sh. milioni 80.

Alisema kwa sasa wameanza kuijenga kwa kuikwangua na kuisawazisha kwanza na kwamba baada ya mwezi mmoja na nusu itakuwa imekamilika na itakuwa inatumika kwa kipindi chote kwa mwaka bila wananchi kukwama. "Kuna kipindi barabara hii ilikuwa inajifunga kabisa, wananchi walikuwa wanaipigia kelele, lakini tulikuwa hatuna namna kwa sababu tulikuwa hatuna pesa za kuifanyia matengenezo na sasa tumezipata na ndiyo maana tumeanza kuijenga," alisema Matindi.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwataka wananchi kuwapuuza baadhi ya wanasiasa wanaohoji ujenzi wa barabara hiyo kufanyika kipindi hiki cha uchaguzi, akidai kuwa serikali haisimamishi kazi zake kwa sababu ya uchaguzi.

Chalamila alisema fedha za ujenzi wa barabara hiyo pamoja na barabara ya Iyela zilitolewa na Rais Dk. John Magufuli baada ya kuombwa kutokana na ubovu wa barabara hizo.

Alisema kwa sasa barabara hizo zinajengwa kwa kiwango cha changarawe, lakini baada ya muda sio mrefu zitaingizwa kwenye mfumo wa ujenzi kwa kiwango cha lami. "Hii barabara tunataka izungukie Iziwa, Nsoho mpaka Itagano, lakini itaendelea mpaka kwenye Kata ya Iwambi na itatumika kama njia ya mkato kwenda Mbalizi," alisema Chalamila.



Baadhi ya mafundi wanaojenga jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya wakiendelea na ujenzi wa nguzo mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Viongozi dini waasa waumini kushiriki vurugu za uchaguzi

**Nebart Msokwa,** MBARALI

VIONGOZI wa dini katika Wilaya ya Mbarali, wamewataka waumini wao kuepuka kushiriki kwenye vitendo ambavyo vinaweza kuhatarisha amani ya taifa hasa kuelekea kwenye siku ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28.

Waliyasema hayo juzi walipokuwa wanazungumza na wandishi wa habari kwenye Mji wa Ubaruku wilayani humo kuhusu hali ya amani wilayani humo ambapo walisema wana taarifa kuwa kuna baadhi ya watu wamejiandaa kuharibu uchaguzi.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Amani ya Wilaya hiyo, Shekh Ayubu Bisiki, alisema Watanzania wote wanatakiwa kushiriki kulinda amani ya nchi ambayo ni tunu iliyodumu kwa muda mrefu akidai kuwa endapo itatoweka kila mmoja atapata madhara.

Alisema kila Mtanzania ana uhuru wa kuchagua kiongozi anayemtaka na hivyo ikifika siku ya uchaguzi kila mmoja anatakiwa aende kwenye kituo alichojiandikisha ili kutimiza haki hiyo kwa kuzingatia maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

"Amani tuliyonayo ndiyo inayotufanya tukusanyike makanisani na misikitini kumwabudu Mungu, sasa kila mmoja wetu anatakiwa kuilinda amani hii, sisi viongozi wa dini ni lazima tuwaelimishe waumini wetu kuilinda amani hii," alisema Shekh Bisiki na kuongeza:

"Tusikubali hata siku moja kugawanywa kwa misingi ya dini zetu, rangi zetu wala namna yoyote ile, wote tupiganie taifa letu uchaguzi usije ukatugawa tukafika hatua ya kupigana."

Aidha, Shekh Bisiki alikanusha taarifa zinazosambaa zikidai kuwa Waislamu wamekubaliana kumpigia kura mmoja wa wagombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Oktoba 28, akidai ni uzushi.Kwa upande wake, Emmanuel Kitundu, Mchungaji wa Kanisa la EAGT na Mjumbe wa Kamati ya Amani, alisema watu wa mataifa mengi duniani yanatamani kuja kuishi Tanzania kwa sababu ya amani iliyopo na hivyo ni muhimu kuilinda.

Alisema katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye uchaguzi mkuu, kila Mtanzania anatakiwa kushiriki kulinda amani kwa kutoa taarifa kwenye mamlaka husika pale wanapoona ama kubaini vikundi au watu ambao wanakusudia kuvuruga amani.

Aliwataka viongozi wa siasa wilayani humo kuepuka kuwahamasisha wananchi kufanya vurugu kwenye uchaguzi na badala yake wajitahidi kuyatumia majukwa yao kuhubiri amani.

"Tumesikia kuna baadhi ya wanasiasa wanawashawishi wananchi kutoondoka kwenye vituo vya kupigia kura wakiwataka wabaki ili kulinda kura zao kitu ambacho ni kinyume na maelekezo ya tume, wananchi wajuwe kwamba risasi huwa haiangalii huyu ni mchungaji, sheikh au raia," alisema Mchungaji Kitundu.





# JK awapigia debe wagombea wa CCM

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS mstaafu wa Tanzania, Jakaya Kikwete, alisema licha ya Tanzania kuwa na mchanganyiko wa watu wenye makabila na dini tofauti, lakini bado wananchi wake wana umoja, upendo, mshikamano na amani.

Aliyasema hayo wakati akiwanadi wagombea ubunge, uwakilishi na udiwani kupitia CCM wa majimbo tisa ya Mkoa wa Mjini Magharib Unguja katika mkutano wa kampeni uliofanyika Viwanja vya Binti Hamrani Jimbo la Mpendae.

Alisema baadhi ya nchi jirani ukabila unawatafuta na imani za kidini kwa wananchi wao zimewagawa na kupelekea uvunjifu mkubwa wa amani.

Kikwete aliitolea mfano kwa Burundi ambayo wananchi wake ni wamakabila mawili ambayo ni Wahutu na Watusi ambao hawaelewani na wakati mwingine hupigana hadi kuuana.

"Baadhi ya nchi za wenzetu wanatuonea wivu kwa sababu Tanzania ina utulivu wa amani... isitoshe Tanzania tuna sera nzuri ambayo inatekelezwa kupitia ilani ya Chama Cha Mapinduzi na sera nzuri zinazozuia udini na ukabila," alisema.

Alieleza kuwa viongozi wa mwanzo waliyoiongoza Tanzania na Zanzibar ambao ni Mwalimu Julias Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume waliweka msingi huo wa utulivu na amani ambapo viongozi waliofuata akiwamo yeye wanazingatia msingi huo.

Aliwataka wananchi wa Tanzania Bara na Zanzibar kuichagua na kukipigia kura CCM katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 kwa sababu kinatengeneza ilani inayotambua na kufuatilia majaribu ya kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

"CCM ipo makini kutekeleza ilani hivyo umahiri, umakini na ubora wa manahoza wake ndicho kitakachoamua ufanisi wa ilani hiyo ndio maana nawaombeni tumchague Dk. Mwinyi kuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Magufuli kuwa rais wa Tanzania na wagombea wote wa CCM majimboni," alisema.

Aliongeza: "Dk. Mwinyi namfahamu vizuri sana, alikuwa waziri wangu kwa muda wa miaka kumi ni kiongozi makini, mwenye hekima, busara, hana papara na ni kiongozi asiye na ajizi kuzungumzia maendeleo ya Zanzibar... ndugu zangu Wazanzibari nawaambia Mwinyi anatosha wengine wa nini?" Alihoji.

Aidha, Kikwete aliwataka wakazi wa Jimbo la Mpendae kumpigia kura mgombea ubunge wa jimbo hilo, Tawfiq Salum Turky, ili kuendeleza yale yote aliyoyafanya marehemu baba yake katika kuwaletea maendeleo wananchi wa jimbo hilo.

Aliwataka wananchi na wana CCM wa majimbo tisa yaliomo katika Mkoa wa Mjini Magharib Unguja kuhakikisha majimbo hayo yote yanakuwa mikononi mwa CCM ikiwamo la Malindi ambalo linaonekana kuwa ni ngome ya wapinzani.

Naye Turky alisema endapo atapata ridhaa ya kuliongoza jimbo hilo, atahakikisha analiletea maendeleo ikiwamo ya elimu, afya, miundombinu na barabara za ndani na kuwawezesha vijana na wanawake kujikomboa kiuchumi.

Alisema ni aibu Shule ya Mpendae iliomo ndani ya jimbo hilo kuwa ni ya mwisho kwa mkufanya vibaya katika matokeo ya mitihani ya kidato cha sita, hivyo atahakikisha shule hiyo inakuwa kinara kwenye mitihani.



Baadhi ya watalii wakiteremka katika ndege ya Shirika la Sky up Airline kutoka Ukraine ikiwa na watalii 215 liyowasili juzi, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kwa ajili ya kufanya shughuli za utalii Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Watalii waanza kumiminika Z'bar baada ya corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADA ya Serikali ya Zanzibar kufungua milango katika sekta ya utalii kutokana na kumalizika kwa ugonjwa wa corona, watalii kutoka mataifa mbalimbali wameanza kuingia Zanzibar kwa wingi.

Juzi ndege aina ya Sky up Airline kutoka Ukraine ikiwa na watalii 215 iliwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kwa ajili ya kufanya shughuli za utalii Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Khamis M'beto, alisema ujio wa watalii hao utasaidia kuinua uchumi wa nchi.

M'beto alisema hayo ni mafanikio makubwa tangu Zanzibar iliporuhusu shughuli za utalii kufuatia kutokomea kwa ugonjwa wa corona.

Alisema ndege nyingine kutoka Urusi inatarajiwa kuwasili Zanzibar wiki ijayo ikiwa na idadi kubwa ya watalii, ambao watatembelea maeneo mbalimbali ya vivutio vilivyopo Zanzibar.

"Tumefungua milango ya kuruhusu watalii kuja nchini baada ya kumalizika kwa ugonjwa wa corona...tunatarajia watalii wengi zaidi kutoka katika nchi za Ulaya na Asia," alisema M'beto.

Naye Ofisa Mwandamizi kutoka Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Haji Ali, alisema wamejipanga vizuri kupokea watalii wanaowasili nchini, huku tahadhari ya ugonjwa wa corona ikiwa imechukuliwa.

Kwa upande wao watalii hao, walisema kuwa wamefika Zanzibar kwa sababu imekuwa ikisifika sana kuwa na vivutio vingi, zikiwamo fukwe nzuri pamoja na mandhari yake.

# Mama wa wenye ulemavu wa mgongo wazi bado waathirika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKATI jana dunia ikiadhimisha Siku ya Ulemavu wa Kichwa Maji na Mgongo Wazi, imeelezwa kuwa bado wanawake wenye watoto wenye ulemavu huo wanakabiliwa na vikwazo vingi.

Miongoni mwa vikwazo hivyo ni kutelekezwa na watoto hao kutokana na mitazamo hasi ya jamii kuhusu ulemavu huo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja Mjini Zanzibar, kuhusu maadhimisho hayo, mama mwenye mtoto wa ulemavu huo, Rahma Mkanga, alisema wanakabiliwa na vikwazo vya malezi ya watoto hao, hivyo ni vyema serikali kuwasaidia kuanzisha vituo vya kulelea watoto wenye ulemavu huo.

Alisema wanakabiliwa na tatizo la unyanyapaa katika jamii na baadhi ya wanawake wenye watoto wenye ulemavu huo, ndoa zao zimevunjika kwa sababu ya waume zao kuwakataa kwa madai ya kuzaa mtoto mwenye kichwa maji na mgongo wazi.

"Baadhi ya wanajimii wanaona kuzaa mtoto mwenye kichwa maji na mgongo wazi ni kama laana, hivyo huwakataa watoto hao na sisi kinamama ndio tunaotupiwa mzigo mkubwa wa malezi," alisema. Naye Ofisa Mawasiliano na Habari wa Asasi ya Child-Help International, Militon Mwijage Byemerwa, alitawaka wazazi na walezi wenye watoto wa ulemavu huo kuwapeleka mapema katika hospitali na vituo vya afya ili kupatiwa matibabu stahiki.

Alisema, uzoefu unaonyesha kuwa ukosefu wa uelewa wa kutosha juu ya maradhi hayo kumepelekea kukosekana takwimu sahihi zinazowahusu watoto hao, hivyo, kuleta ugumu katika kujenga hoja ya kushughulikia tatizo hilo. Alisema hakuna takwimu halisi kuhusiana na ukubwa wa tatizo hilo duniani wakati takwimu kupitia IF&Chil Help Tanzania zikionyesha matukio milioni moja kwa mwaka. Tanzania inakadiriwa watoto watano hadi 10 huzaliwa na tatizo hilo katika kila vizazi 1,000.

Alisema vipo vikwazo kadhaa hasa ukosefu wa taarifa muhimu kwa jamii, hivyo ni muhimu kuelewa ulemavu huo, chanzo, dalili na tiba, ingawa changamoto zinazoambatana na tatizo hilo, bado jamii haijalipa uzito unaostahli.

"Bado tunayo kazi kubwa inayohitajika kama kweli tunahitaji kuliondosha, kuelimisha jamii ni muhimu kwetu sote, taifa na dunia kwa ujumla," alisema.

Aliongeza kwa kusema "Tumegundua kuwapo kwa imani potofu na mambo ya kishirikina kuhusu ulemavu huu, jambo ambalo halina ukweli wowote".

Aidha, alisema, zipo familia zinazosambaratika kutokana na kupata watoto wenye ulemavu huo ambapo waathirika wakubwa ni wanawake kutokana na kutelekezwa na wenza wao.

Byemerwa alisema, matokeo yake, watoto wengi kufichwa majumbani na wengine kutishiwa au kuuawa na baadhi ya wazazi wao au wanafamilia, jambo ambalo halikubaliki na ni kinyume cha haki za binadamu.

"Lishe bora hasa matumizi ya vyakula vyenye wingi wa Foliki Asidi ambavyo vinapatikana maeneo mengi ndio kinga pekee ya mama anayetaka kubeba ujauzito ili asipate mtoto mwenye ulemavu huo," alisema na kuongeza:

"Mfano wa vyakula hivyo ni utumiaji wa mboga, matunda, mazao jamii ya kunde, mihogo, nyama na mayai vinahitajika zaidi kutumika."

Daktari wa wodi ya wagonjwa wa vichwa vikubwa na migongo wazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Seif Khamis Lali, alisema wajawazito wakifika mapema katika hospitali na vituo vya afya kutasaidia kupata matibabu na ushauri wa kina, hivyo kupunguza au kutokomeza kabisa tatizo la watoto wenye vichwa maji na mgongo wazi.

# TAKUKURU yapokea malalamiko 136

**Na Said Hamdani,** LINDI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi, imeokoa Sh. 327,119,853 zikiwamo za wakulima wa korosho, ufuta, miradi mbalimbali ya maendeleo na kodi ya serikali.

Naibu Mkuu wa Taasisi hiyo mkoani hapa, Charles Mulebya, alisema hayo alipokuwa anatoa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, mwaka huu.

Alisema fedha zilizookolewa ni za kipindi cha miezi mitatu na kati ya hizo Sh. 145,143,020 zilirejeshwa serikalini huku Sh. 181,976,833 zikirejeshwa kwa wakulima.

Alisema katika kipindi hicho, ofisi ya taasisi hiyo kupitia dawati la kuzuia rushwa, imefuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo maji na nyumba za kuishi watumishi yenye thamani ya Sh. 1,845,690,295/52.

Mingine iliyotajwa kufuatiliwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa maeneo ya Kata za Chikonji na Rutamba, Halmashauri ya Mtama, Wilaya ya Lindi, Pande, Njia Nne na Somanga katika Wilaya ya Kilwa.

Alisema ufuatiliaji huo umebaini miradi ya maji kwa kata za Pande, Njia Nne, Somanga na Rutamba yenye thamani ya Sh. 1,700,692, 395/52 imebainika kuwa na upungufu, ikiwamo kuchelewa ukamilishaji kama ilivyopangwa.

Pia, alisema, mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa Shule ya Msingi Kata ya Chikonji, wenye thamani ya Sh. 75,000,000 ulikutwa haujakamilika kwa kutofungwa milango, huku kwenye taarifa ikionyesha tayari imekamilika utekelezaji.

Alisema mradi wa ujenzi wa nyumba za kuishi watumishi wa kituo cha afya, kata ya Somanga, Wilaya ya Kilwa, wenye thamani ya Sh. 69,997,900, wakati wa utekelezaji wake ilibainika kutokaguliwa na wahandisi ili kufuatilia ubora wa ujenzi huo.



Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya uhandisi wa umeme na mitambo viwandani na migodini ya Magare jijini Mwanza, Mabula Magangila (katikati), akimkabidhi cheti cha kuhitimu elimu ya sekondari mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Isagehe iliyopo wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wakati wa mahafali ya kidato cha nne mwishoni mwa wiki. Wanaoshuhudia ni mkuu wa shule hiyo, Adolf Kabyemela. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ombi kutokomeza ukatili kwa watoto

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI pamoja na taasisi binafsi wameombwa kuongeza jitihada katika kutokomeza ukatili wanaofanyiwa watoto.

Rai hiyo ilitolewa na Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, kutoka Dawati la Jinsia na Watoto Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Leah Mbunda, katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike, yaliyoandaliwa na Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC).

Mbunda alisema katika kuhakikisha ulinzi wa watoto unakuwapo, dawati hilo limeendelea kujipanga kushughulikia kwa haraka taarifa zote za ukatili zinazoripotiwa katika dawati hilo.

Alisema Mkoa wa Dar Es Salaam una madawati zaidi ya 20 na kwamba wanahakikisha kwamba askari wanaowekwa kushughulikia matukio hayo ni wale waliopatiwa mafunzo katika vituo vikubwa vya polisi ambao wanaamini kwamba wana uwezo na weledi katika taarifa hizo.

"Tunawapongeza sana WLAC wanafanya kazi kubwa ya kutoa elimu katika jamii la sivyo hali ingekuwa mbaya zaidi, na tunashuhudia asilimia kubwa ya wananchi wameelewa na wamepata mwamko wa namna ya kutumia madawati ya jinsia," alisema Mbunda.

Mratibu wa miradi ambayo inahusiana na ulinzi wa wanawake na watoto wa kituo hicho cha Msaada wa Kisheria cha WLAC, Consolata Chikoti, alisema kundi la watoto lipo kwenye hatari ya kufanyiwa hivyo na kwamba serikali na wadau mbalimbali wanawajibu wa kulinda watoto hao.

# Matiko ajinadi kuwatetea wachimbaji wadogo

**Na Timothy Itembe,** TARIME

MGOMBEA ubunge Jimbo la Tarime Mjini, mkoani Mara kupitia CHADEMA, Esther Matiko, amewaomba wapigakura kumchagua kuwatetea bungeni, ikiwamo kuishinikiza serikali kutoa ufadhili kwa wachimbaji wadogo wa madini, hususan dhahabu.

Kauli hiyo aliitoa jana kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika Kibaga kunakochimbwa madini ya dhahabu, ambapo aliomba kuchaguliwa na kwenda kuwasemea bungeni. "Mkinipa ridhaa ya kwenda bungeni nitaenda kuishinikiza serikali ili kutekeleza sera ya madini, ambayo inaitaka serikali kuwapa mikopo wachimbaji wadogo wa madini mikopo na vifaa vya kufanyika kazi kwa lengo la kuinua kipato chenu," alisema Matiko.

Matiko aliongeza kuwa endapo atapewa tena ridhaa ya kuwa mbunge, atahakikisha miundombinu ya barabara ya Kibaga inalimwa na wasafiri wanaenda kusafiri kwa raha na kufanya biashara zao kwa raha.

Naye mgombea udiwani Kata ya Kenyamanyori kupitia CHADEMA, Thomas Burure, alisema akipewa ridhaa ya kuwa diwani ataanza na kipaumbele cha barabara na wapitaji kutembea kwa raha na kutumia gharama nafuu ya usafiri wa abiria na mizigo.

# Wazazi waombwa kusaidia serikali vikwazo vya elimu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZAZI nchini wameaswa kuisaidia serikali katika kutatua baadhi ya changamoto zinazoikabili sekta ya elimu kwa kuunga mkono jitihada za ujenzi wa madarasa na ununuzi wa vifaa vya kufundishia shuleni.

Hatua hiyo imetajwa kuwa itaongeza kasi ya upatikanaji wa elimu bora.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Uhandisi wa umeme na mitambo viwandani na migodini ya Magare ya jijini Mwanza, Mabula Magangila, wakati wa mahafali ya kidato cha nne ya Shule ya Sekondari Isagehe, wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Magangila ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema katika kipindi hiki ambacho serikali inapambana kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya elimu, ipo haja kwa jamii kuiunga mkono kwa kujitolea katika kutatua changamoto zinazozorotesha ustawi wa sekta hiyo muhimu.

Magangila alitangaza uamuzi wake wa kuajili walimu sita wa ziada watakaolipwa mshahara na kampuni yake, ili waweze kusaidiana na walimu wa shule hiyo kufundisha masomo ya sayansi na biashara ili kutatua changamoto ya uhaba wa walimu wa masomo hayo shuleni hapo.

"Binafsi nimefika hapa nilipo kwa kusaidiwa sana na walimu wa ziada kwa kuwa walimu walikuwa hawatoshi. Naomba Mkuu wa shule atusaidie kutafuta walimu wa ziada wenye sifa za kufundisha masomo ya sayansi na biashara. Kampuni ya Magare tupo tayari kuwalipa mishahara yao ili waongeze nguvu wakati tunasubiri serikali ituletee walimu wa kutosha," alisema.

Alisema kampuni hiyo itamalizia ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa matatu katika shule hiyo pamoja na kusaidia ununuzi wa mashine ya kisasa ya kudurufu, kichapishi( Printer) na kompyuta kwa ajili ya kusaidia shughuli za maandalizi ya mitahani ya wanafunzi hao, huku pia akitoa mchango wa fedha taslimu kiasi cha shilingi milioni moja kwa ajili ya kufikisha mtandao wa majisafi na salama katika shule hiyo.

# NMB yashinda tuzo ya huduma bora

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya NMB imeshinda tuzo ya umahiri wa utoaji wa huduma bora na salama zaidi za kibenki nchini.

NMB imeshinda tuzo hiyo ambayo hutolewa kila mwaka kwa kila nchi na Jarida la Kimataifa la Global Finance la jijini New York nchini Marekani.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Ruth Zaipuna, alisema siri ya benki hiyo kuibuka mshindi ni kutokana na uwezo wake wa kukopesha, afya ya mizania, ukubwa wa mtaji, na udhibiti wa uhalifu wa kimtandao.

Nyingine alisema ni usalama wa huduma za kidijitali, usambazaji wa huduma za kibenki, teknolojia na ubunifu katika kutoa huduma mbadala za kibenki.

"Tuzo za benki salama zaidi hufanywa kila mwaka katika kila bara na kwa kila nchi duniani na hutolewa baada ya kufanya tathmini ya kina kuzingatia viwango vya kampuni za Moody's , Fitch na Fortune 500, vigezo hivi ni vya kimataifa vinavyotoa taarifa za afya za benki na kampuni kujiendesha," alisema Zaipuna.

"Tuzo hii imekuja miezi michache baada ya Benki ya NMB kutunukiwa tuzo ya kuwa benki bora zaidi Tanzania kwa awamu nane mfululizo iliyotolewa na Jarida la Euromoney lenye makao makuu yake jijini London nchini Uingereza linalochapisha habari za masoko ya fedha na mitaji."

"Hii ni heshima kubwa kwetu kutambulika kama benki salama zaidi na yenye uwezo wa kuendelea na biashara kwa ajili ya kuleta faida kwa wanahisa wetu na nchi kwa ujumla. Ni ishara ya uimara wa benki na ubora wa kuhudumia wateja katika soko lenye ushindani na mazingira yanayobadilika kila wakati," alisema Zaipuna.

"Taarifa za fedha za Benki ya NMB zinaonyesha kwa mwaka 2019 ilipata faida ya Sh. bilioni 142 kabla ya kodi ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 46 kutoka Sh. bilioni 98 iliyopata mwaka uliotangulia, hivyo kuifanya iendelee kuwa benki inayoingiza faida kubwa zaidi nchini kwa zaidi ya muongo mmoja sasa."

Joseph Giarraputo, Mhariri Mkuu wa Jarida la Global Finance, alisema janga la corona limeathiri sehemu kubwa ya biashara kwa mwaka huu na hivyo kufanya makisio duniani kuwa magumu.

# Ofisi CHADEMA Shinyanga yanusurika kuwaka moto

**NA MARCO MADUHU,** SHINYANGA

OFISI ya CHADEMA Kanda ya Serengeti iliyopo Shinyanga Mjini, imedaiwa kunusurika kuchomwa moto na watu ambao hawajajulikana.

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Serengeti, Jackson Mnyawami, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana, majira ya saa 7 usiku.

Alisema watu hao walivunja dirisha la kioo lilipo upande wa ofisi yake, na kisha kutupia dumu la lita moja na nusu likiwa na petroli ndani, kwa ajili ya kuwasha moto, lakini walishindwa baada ya kukurupushwa na mlinzi.

"Tunalaani tukio hili la kutaka kuchomwa moto ofisi yetu ambayo ina jumuisha mikoa ya Mara, Simiyu, na Shinyanga, tunaomba Jeshi la Polisi lifanye kazi yake, ili libaini watu ambao walitaka kufanya tukio hili ambalo ni baya sana hasa katika kipindi hiki cha uchaguzi," alisema Mnyawami.

"Pia tunaomba wafuasi wa vyama mbalimbali vya siasa, kwa siku hizi zilizosalia kupiga kura, tufanye siasa za kistaarabu kwa kunadi sera za wagombea wetu, na siyo kufanyiana fujo ambazo hazina maana na kuhatarisha amani ya nchi yetu," aliongeza.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, na kueleza uchunguzi unafanyika kubaini wahusika wa tukio hilo, ili wachukuliwe hatua kali za kisheria.



Meneja Rasilimali Watu na Maendeleo wa Vodacom Tanzania PLC, Naiman Moshi, akiongea na wahitimu wa mafunzo ya ubunifu wa Website "Women in Data Science Dar es Salaam 2020" yaliyoandaliwa na Tanzania Data Lab kwa udhamini wa Vodacom Tanzania PLC kupitia programu yake ya 'Code like a girl' yaliyowashirikisha wanafunzi wa kike kutoka jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yazionyesha taasisi za fedha miradi ya kuwekeza

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imezishauri taasisi za fedha kuwekeza katika maeneo ambayo yatasaidia kukuza uzalishaji kwa ajili ya kuuza bidhaa nje ya nchi.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri MKuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, alipotembelea benki za NBC, TPB, NMB na TIB kwa ajili ya kuangalia utendaji wa taasisi hizo upande wa uwekezaji.

Alizitaka taasisi hizo kuwekeza kwenye miradi muhimu ya uzalishaji ambayo itaisaidia nchi kuondokana na utegemezi wa kununua bidhaa nje ya nchi kwani zitakuwa zikitengenezwa hapahapa.

Waziri Kairuki alitaja maeneo muhimu ambayo taasisi hizo zinaweza kusaidia kuwekeza kuwa ni pamoja na ujenzi wa viwanda vidogo na vikubwa na utengenezaji wa dawa.

"Kuna aina karibu 700 za dawa na vifaa tiba, hivyo naona ni eneo muhimu sana la kuwekeza ambalo watu wa benki wanatakiwa kuliona kama sehemu ya kuwekeza," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), Revocatus Rasheli, alitoa wito wa ushirikiano kati ya taasisi za fedha na taasisi hiyo katika kuhimiza uwekezaji kwenye maeneo mbalimbali.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa TIC, Dk. Maduhu Rasheli, alisema pia itakuwa muhimu kwa taasisi za fedha kutangaza huduma wanazotoa kwenye majarida yanayotolewa na kituo hicho ili kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo.

## Tigo yaja na 'Jaza Tukujaze Tena'

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mawasiliano inayoongoza kwa kutoa huduma za kidigitali nchini Tanzania, Tigo, leo (Jumatatu) imezindua kampeni ya siku 90 itakayofanyika nchi nzima ambayo imelenga kuwafanya wateja wote wa Tigo kuwa washindi wa zawadi mbalimbali kila wanaponunua bando za siku, wiki au mwezi.

Kampeni hiyo iliyopewa jina la 'Jaza Tukujaze Tena' inalenga kuwazadia wateja kutokana na uaminifu wao kwa kampuni ya Tigo, hivyo ndani ya kipindi cha kampeni, wateja wataweza kuzawadiwa dakika za muda wa maongezi, SMS, pamoja na MBs/GBs kila watakoponunua bando.

Pia, mbali na wateja kuzawadiwa muda wa maongezi pamoja na MBs za bure, kutakuwa na simu janja zaidi ya 1,200 ambazo pia watazawadiwa wateja.

Simu janja zitakazoshindaniwa ni pamoja na Samsung Note 20, ITEL T20 pamoja na Smart Kitochi. Simu janja hizi zitashindaniwa na wateja wote wa Tigo, mawakala, viongozi wa timu za mauzo na wahudumu wakubwa wa Tigo Pesa.

# GUARDIOLA: CITY INAPITIA WAKATI MGUMU SASA



**LONDON,** England

PEP Guardiola amesisitiza Manchester City wanafanya "kwa uhakika kila kitu" katika mazingira magumu wakati walipolazimishwa sare ya kufungana bao 1-1 na West Ham kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England, Jumamosi.

Phil Foden alitokea benchi na kusawazisha bao la Michail Antonio, lakini City hawakuwa na uwezo wa kuibuka na ushindi kwenye mchezo huo, wakati Raheem Sterling na Riyad Mahrez waliposhindwa kutumia nafasi zao za dakika za majeruhi kufunga mabao.

Kupata pointi tisa katika mechi tano ni mwanzo mbaya zaidi kwa klabu hiyo tangu msimu wa 2014-15, wakati walipokabiliwa na wakati mgumu huku wao wakiwa mabingwa watetezi chini ya Manuel Pellegrini.

Foden aliingia dimbani kuchukua nafasi ya Sergio Aguero, ambaye aliumia misuli akiwa ameanza katika mechi tatu tu tangu arudi kutoka kuuguza majeraha.

Aguero alianzishwa kwenye mchezo huo kwa sababu Gabriel Jesus aliwekwa benchi, huku walinzi, Aymeric Laporte, Nathan Ake na Benjamin Mendy wote hawakuwapo kwenye mchezo huo uliopigwa pale jijini London.

Fernandinho anatarajiwa kuwa nje ya dimba kwa wiki sita baada ya kuumia Jumatano kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wakiibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Porto, huku Laporte, Mahrez na Ilkay Gundogan wote walikutwa na maambukizi ya virusi vya corona msimu huu.

"Ningepeda kuwa na matokeo, lakini ukiangalia hali halisi, mambo ni magumu sana kwetu," alisema akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Tunapata tabu sana kwa sababu tuna majeruhi wengi na wengi hawajapona kwa wakati na tuna mechi nyingi ngumu na muhimu mbele yetu.

# Klopp amtabiria makubwa Jota

**LIVERPOOL** England

JURGEN Klopp anaamini Diogo Jota atakuwa bora zaidi kwa Liverpool baada ya kufunga bao la ushindi dhidi ya Sheffield United kwenye Ligi Kuu, Jumamosi.

Jota alifunga bao hilo la ushindi dakika ya 64 pale kwenye dimba la Anfield, ambao mabingwa hao watetezi walitoka nyuma, wakihitaji bao la Roberto Firmino kusawazisha lile la Sander Berge alilofunga kwa mkwaju wa penalti.

Akiwa amesajiliwa kutoka Wolves mnamo Septemba kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 41, Jota alikuwa mchezaji wa kwanza wa Liverpool tangu Sadio Mane mwaka 2016 kufunga katika mechi zake zote mbili za ufunguzi za Ligi Kuu nyumbani kwa klabu hiyo.

Klopp alimwanzisha Jota na utatu wake wa kawaida pale mbele, Mane, Mohamed Salah na Firmino na kocha huyo wa Liverpool alikuwa na furaha kubwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.

"Ni mtu ninayempenda. Ni rahisi sana kumpenda na anafanya kila kitu kuwa rahisi hapa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.






# Koeman alia VAR inaiua Barca

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman amesema mfumo wa Teknolojia ya Usaidizi wa Maamuzi kwa njia ya Video (VAR), inaonekana tu "kutumiwa kufanya maamuzi dhidi ya Barcelona."

Koeman alionekana kutoridhishwa na maamuzi ya VAR baada ya kuamua penalti wakati Barcelona ikichezea kichapo cha mabao 3-1 kwenye mchezo wa 'Clasico' dhidi ya Real Madrid, Jumamosi katika Uwanja wa Camp Nou.

Mlinzi na nahodha wa Real Madrid, Sergio Ramos, aliyepanda kusaidia mashambulizi alionekana kuvutwa jezi na kudondoshwa eneo la hatari na mwamuzi akalazimika kwenda kuhakikisha faulo hiyo kwenye VAR.

Na Ramos akafunga penalti hiyo kuipa Real Madrid bao la pili baada ya Federico Valverde kufunga la uongozi kabla ya Ansu Fati mwenye umri wa miaka 17, kusawazisha na kuweka rekodi ya mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kufunga historia ya mchezo wa Clasico.

Na Luka Modric aliyeingia kipindi cha pili akafunga bao la tatu kwa Real Madrid na kuwapaisha hadi kileleni mwa msimamo. Koeman baada ya mchezo huo alisema VAR mara zote ipo kwa ajili ya kuimaliza Barcelona.

"Nafikiri VAR inatumiwa kufanya maamuzi dhidi ya Barcelona tu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulifanyiwa faulo nyingi na kunyimwa penalti mbili, lakini VAR haikufanya kazi, kwa sababu ni Barcelona, lakini ikiwa dhidi yetu inafanya kazi vizuri sana. Hongera kwa VAR."

## HABARI MICHEZO

# De Gea asikitika Man Utd kuikosa Chelsea EPL

**MANCHESTER,** England

DAVID de Gea anaamini Manchester United walistahili zaidi kupata ushindi kuliko Chelsea baada ya timu hizo mbili kumaliza mchezo bila kufunga, Jumamosi.

Mchezo huo ulikuwa ni wa tano kwa United msimu huu, huku ikiwa imeshinda mechi mbili tu tangu kuanza kwa msimu huu.

Golikipa wa Chelsea, Edouard Mendy alifanya kazi ya ziada kuokoa mara mbili mashuti ya Marcus Rashford, ikiwamo dakika ya mwisho na pia Bruno Fernandes.

Kwa kufanya hivyo, golikipa huyo raia wa Senegal amekuwa golikipa wa kwanza wa Chelsea kucheza ugenini kwa United bila nyavu zake kutikiswa tangu Thibaut Courtois, Desemba 2015.

Na De Gea anahisi kikosi chake kilifanya kazi nzuri na kilistahili pointi tatu na si moja ambapo sasa wapo nafasi ya 15 kwenye msimamo baada ya michezo mitano.

"Kwangu mimi, tulitengeneza nafasi nyingi za kushinda mchezo. Ulikuwa mchezo mgumu dhidi ya timu nzuri bila shaka yoyote, lakini nafikiri tulistahili kushinda," alisema akiiambia MUTV.

"Nafikiri tulikuwa na nafasi mbili au tatu kubwa, hasa kwa Rashy, lakini golikipa aliokoa zote.

"Hilo sawa, kama nilivyosema hapo awali, tulistahili kushinda mchezo huu kwa namna yoyote."





# LUKAKU ANANIPA RAHA INTER-CONTE

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amesifia kuimarika kwa Romelu Lukaku wakati nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji akicheza kwa kiwango cha kuvutia na kuisaidia Inter Milan kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Genoa kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie, Jumamosi.

Lukaku alifikisha bao la 10 katika mechi nane msimu huu kwa klabu na nchi yake wakati alipowaweka mbele Inter katika mchezo huo uliopigwa dimba la Luigi Ferraris kabla ya Danilo D'Ambrosio kuongeza la pili na kuwavuta hadi nafasi ya tatu kwenye msimamo.

Straika huyo wa zamani wa Manchester United, sasa ana mabao 22 kwa Inter tangu alipoanza kucheza kwenye Serie A, Agosti 2019, ukitoa yale ya penalti, ambao ni mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote wa kigeni kwenye ligi hiyo.

Conte amesema kwa muda mrefu alikuwa akivutiwa na Lukaku na anafuraha namna anavyoimarika kwa kiwango chake kwa miezi 12 iliyopita.

"Romelu ni mchezaji wa tofauti na yule wa mwaka mmoja uliopita," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Mara zote nilisema hapo mwanzo, alikuwa almasi chafu na ndio maana nilitaka kufanya naye kazi.

"Anafanya vizuri na unaweza kuona namna anavyocheza na kuisaidia timu kusukuma mpira mbele. Ameimarika kwa kila kitu."

# *Lewandowski aahidi kufunga zaidi Bayern*

**MUNICH,** Ujerumani

ROBERT Lewandowski ameapa kuendelea kufunga zaidi wakati mabao yake matatu 'hat-trick' yaliisaidia Bayern Munich kuifumua Eintracht Frankfurt 5-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Jumamosi.

Lewandowski, ambaye alifunga mabao 34 kwenye mechi 31 za Ligi Kuu msimu uliopita, tayari amefikisha mabao 10 katika mechi tano msimu huu, akiweka rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi kwa mechi za awali kuliko mchezaji yeyote kwenye mashindano hayo.

Aliifungia Bayern mara mbili ndani ya dakika 26 na alikamilisha hat-trick yake katika kipindi cha pili kabla ya kuingia kwa Leroy Sane na Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 17, ambao kila mmoja alifunga moja.

"Mara zote tunataka kucheza soka bora. Wakati tukiwa na nafasi ya kushinda kama leo (juzi), tunaamua iwe mapema zaidi," alisema Lewandowski.

"Baada ya ushindi wa 3-0 tuliamua mchezo, halafu tukawa tunajiachia kwa kucheza tunavyotaka.

"Kwa upande wangu kila nikipata nafasi nitakuwa nafunga na ndivyo ninavyotaka na kwa uhakika tunataka timu iendelee kuwa bora kila siku."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ZIDANE ACHAMBUA USHINDI KWA BARCA

## ●●● Linapokuja suala la kulinda, tulikuwa vizuri na kuzuia mashambulizi yote na kwa timu kama...

**BARCELONA,** Hispania

ZINEDINE Zidane amesisitiza hakuwa na nia ya kuzima uvumi wa majaliwa yake hapo Real Madrid baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 kwenye mchezo wa Clasico dhidi ya Barcelona, Jumamosi.

**Baada ya Ansu Fati kusawazisha bao la Federico Valverde la ufunguzi, Sergio Ramos alifunga kwa penalti dakika ya 63 na Luka Modric akaihakikishia ushindi Madrid pale kwenye dimba la Camp Nou.**

Zidane alikuwa kwenye presha kubwa baada ya kupoteza mechi mbili mfululizo, akianza kwa Cadiz na kufuatiwa na Shakhtar Donetsk kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini Madrid ikajivuta kileleni mwa msimamo wa LaLiga baada ya ushindi wa Jumamosi.

Na kocha huyo wa Real Madrid alisema hakuwa na nia ya kujaribu kujibu mashambulizi kuhusu shutuma dhidi yake.

"Hatupo hapa kwa ajili hiyo, kuwanyamazisha wao," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari.

"Tunafanya kazi yetu, tukiamini kile tunachokifanya, kuwa pamoja pale inapobidi kupambana pamoja na ndicho tulichofanya. Tulifanya hivyo kama timu, najivunia sana vijana wangu. "Linapokuja suala la kulinda, tulikuwa vizuri na kuzuia mashambulizi yote. Na kwa timu kama Barca, tulilazimika kucheza kwa kujihami maana aina ya uchezaji wao ni ngumu kidogo kuwadhibiti kiurahisi, lakini tulifanikiwa."

Madrid sasa imeshinda mechi nne kati ya sita za Ligi Kuu ya Hispania msimu huu.

"Tulicheza mchezo mzuri, kucheza na timu ambayo tunaijua inafungana sana, sisi tulikuwa kwenye kiwango bora," alisema.

"Nina furaha kwa wachezaji kwa sababu mwisho wa mchezo kilichokuwa kinatakiwa ni ushindi tu, hasa baada ya siku chache za kufanya vibaya. Nina furaha juu yao na bao la Modric lilikuwa bora zaidi.

"Niliona timu ikicheza kwa umoja. Nina furaha kwa sababu walionyesha ari ya kupambana uwanjani. Tunafurahia kile tulichokifanya."

Madrid itasafiri kwenda kucheza na Borussia Monchengladbach nchini Ujerumani kwenye mchezo wa pili wa makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kesho Jumanne, kabla ya kuwavaa Huesca siku nne baadaye kwenye Ligi Kuu.

## ZISIKUPITE

### LIVER YAJIPANGA KWA OZAN

LIVERPOOL imefungua mazungumzo na Schalke usajili wa dirisha dogo la Januari wa pauni milioni 20 kwa mlinzi wa Uturuki, Ozan Kabak, 20, baada ya kuumia kwa muda mrefu kwa Virgil van Dijk. ***(Sunday Mirror)***

### WILSHERE KWENDA MAREKANI

KIUNGO wa zamani wa Arsenal na England, Jack Wilshere, 28, anakaribia kwenda kucheza Ligi Kuu ya Marakeni (MLS), wakati akitafuta klabu mpya baada ya kuondoka West Ham. ***(Sunday Mirror)***

### ROMERO KUSEPA MAN UTD

GOLIKIPA wa Manchester United, Sergio Romero, raia wa Argentina anapanga kufanya mazungumzo na kutaka kuondoka Old Trafford. Kipa huyo mwenye umri wa miaka 33, ana matumaini makubaliano yanaweza kufikiwa ya kufunga mkataba wake ili atafute timu nyingine. ***(Star on Sunday)***

### MADRID, POCHETTINO WATETA

REAL Madrid imewasiliana na kocha wa zamani wa Tottenham na Southampton, Mauricio Pochettino kuhusu uwezekano wa kuchukua nafasi ya Zinedine Zidane. ***(El Transistor)***

### LEEDS YAMWANIA MCGURK

LEEDS wanataka kujaribu kumsajili kiungo wa Wigan, Sean McGurk, mwenye umri wa miaka 17, wakati wa dirisha dogo la usajili Januari. ***(Sun)***

### 'WHITE HAENDI LIVERPOOL'

KOCHA wa Brighton, Graham Potter, amekanusha uvumi kwamba mlinzi wake, Ben White, 23, anahusishwa na mpango wa kusajiliwa na Liverpool. ***(Sunday Mirror)***

### ATAKA KUSAJILI ZAIDI

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, amemtaka Mwenyekiti wa klabu hiyo, Daniel Levy, kumuunga mkono kwenye usajili kama ambavyo Liverpool imefanya katika miaka ya hivi karibuni. ***(Sunday Express)***

### MOORE AGOMBEWA EPL

KLABU za Wolves, West Ham, Crystal Palace, Southampton na Newcastle zote zinamfuatilia nahodha wa Reading, Liam Moore, mwenye umri wa miaka 27 ili kumsajili. ***(TeamTalk)***

### SOLSKJAER AMTULIZA DE BEEK

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amemhakikisha kiungo wa Uholanzi, Donny van de Beek, 23, muda wake unakuja hapo Manchester United baada ya kutomtumia katika sare ya bila kufungana dhidi ya Chelsea, Jumamosi. ***(Manchester Evening News)***

### AJUTA KUMUUZA BREWSTER

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema kumuuza straika Rhian Brewster, 20, kwenda Sheffield United "ulikuwa wakati mgumu sana". ***(Sunday Express)***

### BERTRAND, UBAGUZI WA RANGI

MLINZI wa kushoto wa Southampton, Ryan Bertrand, mwenye umri wa miaka 31, amepewa sapoti kwenye Ligi Kuu England kwenye kampeni ya ubaguzi wa rangi, baada ya kubainisha kwamba alinyanyaswa sana wakati wa utoto wake. ***(Sunday Mirror)***

## HABARI MICHEZO




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (katikati), akikabidhi mfano wa hundi ya thamani ya Sh. milioni 300 kwa Rais wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Anthony Mtaka, ikiwa ni ufadhili wa benki hiyo kwa shirikisho hilo katika kipindi cha miaka mitano ikiwamo kuendesha mbio za NBC Marathon, zinazotarajiwa kufanyika Novemba 22, mwaka huu jijini Dodoma. Makabidhiano hayo yalifanyika jijini Dar es Salaam jana, wakati wa hafla ya uzinduzi wa mbio hizo. Wanaoshuhudia ni pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Dk. Julius Mwaiselage (kushoto). **MPIAGAPICHA WETU**

# MBIO ZA NBC MARATHON ZAZINDULIWA

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa kushirikiana na Shirikisho la Riadha Taifa (RT), wamezindua rasmi mbio zinazofahamika kwa jina NBC Marathon, zinazotarajiwa kufanyika Novemba 22, mwaka huu jijini Dodoma.

**Pamoja na kukuza mchezo huo nchini, mbio hizo pia zinalenga kuchochea mapambano dhidi ya ugonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi nchini, kwa mujibu wa waandaji hao.**

Hafla ya uzinduzi wa mbio hizo ilifanyika jijini Dar es Salaam jana na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, wadau wa mchezo huo wakiwamo viongozi waaandamizi wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), maofisa waandamizi wa benki ya NBC pamoja na vyombo mbalimbali vya habari.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema pamoja na dhamira yao ya dhati ya kuwekeza kwenye mchezo wa riadha kupitia mbio hizo, mapato yote yatokanayo na usajili wa wawakimbiaji yataelekezwa kwenye vita dhidi ya ugonjwa wa saratani ya shingo ya uzazi kupitia Taasisi ya Saratani ya Ocean Road.

"Tumeamua kuelekeza nguvu zetu katika mapambano hayo tukitambua kwamba ugonjwa huu ndio unaoongoza kwa vifo vya saratani hapa nchini. Hivyo, mbio hizi za NBC Dodoma Marathon zitakuwa jukwaa zuri la kusambaza ufahamu juu ya ugonjwa huu ambao tunaambiwa kwamba ukiwahiwa unatibika," alisema.

Katika hafla hiyo pia ilishuhudiwa benki hiyo pamoja na Shirikisho la Riadha Tanzania (RT) wakisaini mkataba wenye thamani ya Sh. milioni 300 ikiwa ni ufadhili wa benki hiyo katika ya kuendesha mbio hizo katika kipindi cha miaka mitano.

"Ni maono yetu kwamba NBC Dodoma Marathon ndio mbio ambazo zitapeperusha jina la NBC katika miaka ijayo, na hivyo tunadhamiria kuendelea na mbio hizi kwa kipindi cha miaka mitano."

"Zaidi ni matumaini yetu kwamba uwekezaji wetu kwenye mchezo wa riadha utatumika vizuri na hivyo kuleta mafanikio kwa wanariadha wetu na kwa nchi yetu kwa ujumla katika siku za usoni," Sabi aliongeza kuwa usajili wa mbio hizo tayari umeanza kupitia matawi ya benki hiyo kote nchini sambamba na mitandao ya kijamii ya benki hiyo.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Rais wa RT, Anthony Mtaka, pamoja na kuipongeza benki hiyo kwa kuamua kuwekeza kwenye kuinua mchezo huo nchini, alisema lengo ni kuzifanya mbio hizo kuwa za mfano na zenye utambuzi wa kimataifa (International Recognition).

"NBC Dodoma Marathon zitakuwa za Km. 5, Km. 10, Km. 21 na Km.42, kwa kuwa lengo ni kuzifanya zitambulike kimataifa, tumehakikisha kwamba njia zote zinapimwa na mpimaji anayetambulika na Shrikisho la Riadha la Dunia (World Athletics). Zoezi hilo la kupima lilikamilika Oktoba 17, mwaka huu jijini Dodoma. Kwa sasa tunasubiri vyeti kutoka Shrikisho la Riadha la Dunia kuthibitisha utambuzi huo," alibainisha.

Alisema uamuzi wa mbio hizo kufanyika jijini Dodoma ulizingatia sababu za msingi kadhaa ikiwamo mandhari ambayo ni kivutio kwa wakimbiaji, mpangilio wa barabara ambazo haziingiliani na barabara kuu na hivyo kuwa salama kwa wakimbiaji wa aina zote.

"Lakini pia tuliona Jiji la Dodoma, kama mji wetu mkuu, unastahili kuwa na tukio kubwa la mchezo unaotambulika kimataifa. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba uamuzi wetu wa kupeleka mbio hizi Dodoma ulikuwa sahihi," alisema.

## Hitimana auona muunganiko Namungo

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Thiery Hitimana, amesema timu yake imeanza kuwa na muunganiko mzuri hali ambayo inampa matumaini ya kufanya vizuri katika michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana alisema ameona muunganiko wa timu yake katika mechi mbili za mwisho walizocheza dhidi ya Kagera Sugar kwa kushinda mabao 2-1 na dhidi ya Ihefu FC waliocheza juzi nakutoka sare tasa.

Alisema ana imani ya kupata matokeo mazuri katika mechi zao zijazo kulingana na mwelekeo wa timu yake kwa wachezaji kuanza kuelewana uwanjani.

Alisema wanarejea nyumbani kufanyia kazi kasoro hizo katika safu ya ushambuliaji ili kuhakikisha nafasi wanazopata wanazitendea haki kwa kupata ushindi wa mabao mengi.

"Sasa tunarejea nyumbani, baada ya kupata pointi moja dhidi ya Ihefu, tunaenda kujiandaa na mechi yetu ijayo dhidi ya Dodoma Jiji FC, nina imani na wachezaji wangu kufanya vizuri kwa mechi zetu zijazo," alisema Hitimana.

Alisema hana majeruhi kwa kikosi kilichorejea kutoka Mbeya na kwamba kipo fiti kupambana kupata pointi tatu katika mechi yao ijayo dhidi ya Dodoma Jiji FC.




Mashabiki wa soka wa Real Madrid na Barcelona, wakipozi katika kombe la mfano la Ligi Kuu Hispania wakati wa shughuli ya Kampuni ya Kubahatisha ya M-Mbet iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# *Mashabiki wa Madrid, Barca wazawadiwa*

**Na Mwandishi Wetu**

USHINDI wa mabao 3-1 wa Real Madrid dhidi ya mahasimu wao, Barcelona umenogeshwa na chemsha bongo ya Kampuni ya Michezo ya Kubahatisha ya M-Bet Tanzania na mashabiki wa soka kujishindia zawadi mbalimbali.

Tukio hilo lilifanyika kwenye Baa ya Tips Mikocheni ambapo mbalimbali ya mashabiki kuzawadiwa zawadi mbalimbali zikiwamo jezi halisi 'orijino' za timu hizo mbili, pia walipata fursa ya kupiga picha na mfano wa Kombe LaLiga ambalo Real Madrid ilishinda msimu uliopita.

Mabao ya Real Madrid katika mechi hiyo ya juzi, yalifungwa na Federico Valverde, Sergio Ramos (kwa njia ya penati) na Luka Modric wakati lile la kufutia machozi la Barcelona lilifungwa na Ansu Fati.

Meneja Masoko wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, Allen Mushi, alisema wameamua kuwachangamsha mashabiki wa soka Ligi ya Hispania kutokana na ushirikiano wao na La Liga.

Mushi alisema wamefikia uamuzi wa kuwazawadia mashabiki wa soka kama kutambua mchango wao katika shughuli zao za michezo ya kubahatisha.

Alisema maswali yao mengi yamelenga ufahamu kuhusiana na LaLiga kama mchezaji gani aliyefunga mabao mengi, wachezaji maarufu waliocheza ligi hiyo, mchango wa Cristiano Ronaldo na Lionel Messi katika timu zao, umaarufu wao na makocha.

"M-Bet imeingia mkataba na LaLiga katika kuendeleza soka la vijana ili kuleta maendeleo ya soka kwa timu zetu na timu ya Taifa, kabla ya kuanza kuendesha mafunzo mbalimbali, tumeamua kuanza kutoa zawadi kwa mashabiki.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 26, 2020

Nipashe




Zidane achambua ushindi kwa Barca UKURASA 22

# YANGA MWENDO MDUNDO LIGI KUU

## ●●● Yazidi kuikimbiza Azam FC, Waziri Junior akitangaza ufalme Kirumba kwa...

**Na Adam Fungamwango**

WAZIRI Junior jana alifunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu Bara msimu huu akiwa na klabu yake mpya ya Yanga kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza, akiifanya kutembea 'mwendo mdundo' kwa kuondoka na pointi zote tatu wakati ikishinda mabao 2-1 dhidi ya KMC FC.

Waziri ambaye alijiunga na Yanga akitoka Mbao FC, alifunga bao hilo kwa kichwa, akiunganisha kona iliyochongwa na Farid Mussa dakika ya 61 ya mchezo kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara na baada ya kufunga alionyesha fulana yake ya ndani iliyoandikwa "The King of CCM Kirumba" (Mfalme wa CCM Kirumba), hiyo ikitokana na msimu uliopita wakati akiichezea Mbao FC kufunga mabao mengi wakati wakiutumia uwanja huo.

**Kwenye mechi hiyo, Yanga ilishtukizwa kwa kufungwa bao dakika ya 26 likifungwa na Hassan Kabunda kwa shuti kali nje ya 18.**

Mfungaji alipata pasi ndefu kutoka kwa Israel Patrick na kuwahadaa mabeki wa Yanga, kabla ya kuachia shuti kali lililomshinda kipa Metacha Mnata na kujaa wavuni.

Kabla ya bao hilo, KMC ilianza kulitia msukosuko lango la Yanga dakika ya 15, lakini shuti la Kenny Ally lilitoka nje kidogo ya lango.

Yanga ilijibu dakika ya 22 wakati krosi ya Kibwana Shomari nusura izae bao, lakini mastraika wa Yanga, Waziri na Michel Sarpong wote waliruka juu na kupiga hewa badala ya mpira, ambao ukatoka nje.

Dakika mbili baadaye shuti la Sarpong lililokuwa kilielekea golini lilimgonga mchezaji mwenzake wa Yanga na kurejea uwanjani, sekunde chache kabla ya shuti la Deusa Kaseke kutoka nje la lango.

Kabunda aliipatia KMC bao la kuongoza dakika ya 26, baada ya kupata pasi ndefu kutoka kwa Israel Patrick na kuwahadaa mabeki wa Yanga, kabla ya kuachia shuti kali lililomshinda kipa Metacha na kujaa wavuni. Feisal Salum, nusura aifungie Yanga bao, baada ya kombora lake kali kugonga mlingoti wa juu na kurejea uwanjani dakika ya 38.

Yanga ilisawazisha bao lake kwa njia ya penalti, baada ya Sarpong kumuhadaa mwamuzi kwa kujiangusha akiwa ndani ya eneo la hatari na Tuisila Kisinda akaijaza wavuni, akimzidi ujanja Juma Kaseja anayesifika kwa kuokota penalti.

Hii ni mara ya pili kwa Kaseja msimu huu kupigiwa penalti, kwani kwenye mechi kati ya timu yake na Coastal Union, aliokoa penalti iliyopigwa na Yusuph Soka mechi ambayo aliisaidia timu yake kutoka sare ya bao 1-1. Kipindi cha pili, hakukuwa na kosakosa nyingi, badala yake timu zote zilionekana kucheza kwa wasiwasi zaidi na kushindwa kutengeneza nafasi.

Kwa matokeo hayo, Yanga bado imeendelea kung'ang'ania kwenye nafasi ya pili, ikifikisha pointi 19 nyuma ya vinara Azam FC ambao leo wanashuka kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro kucheza dhidi ya Mtibwa Sugar ikiwa na pointi 21, zote zikiwa zimecheza mechi saba.

KMC inabakia na pointi zake 11, ikiwa imecheza mechi nane.

Katika mechi zingine zilizopigwa jana Polisi Tanzania ilikubali kipigo cha 1-0 kutoka kwa Biashara Mara United katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha wakati Mwadui FC ikilala kwa mabao 6-1 dhidi ya JKT Tanzania.

HAKUNA PENALTI...!



Beki wa Manchester United, Harry Maguire, akimdhibiti Cesar Azpilicueta kwa kumrukia mgongoni ndani ya eneo la 18, tukio ambalo Chelsea walitoka uwanjani wakilalamika kunyimwa penalti katika mchezo huo wa Ligi Kuu ya England uliopigwa Uwanja wa Old Trafford, timu hizo zikitoka sare tasa juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Bocco, Chama kuituliza Simba leo

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuwakosa washambuliaji wake nguli katika mechi iliyopita, Kocha Mkuu wa Simba , Sven Vandenbroeck, anaweza kumtumia straika John Bocco katika mechi dhidi ya Ruvu Shooting katika Uwanja wa Uhuru leo.

Lakini kiungo mnyumbulifu Clatous Chama naye atakuwa tayari kucheza baada ya kuikosa mechi iliyopita mjini Sumbawanga wakati wakichezea kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Tanzania Prisons.

Bocco pamoja na washambuliaji wenzake Meddie Kagere na Chris Mugalu, wote walikuwa majeruhi, hivyo Sven kulazimika kumtumia Charles Ilamfya ambaye alishindwa kufurukuta ngome ya ulinzi ya Prisons Alhamisi iliyopita katika Uwanja wa Nelson Mandela.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, alisema kwa mujibu wa Daktari wa Simba, Yassin Gembe, Bocco anaweza kucheza kama atakuwa katika mipango ya mwalimu.

"Bocco amesharejea na amekuwa akifanya mazoezi na wenzake, hivyo kucheza ama kutokucheza itategemea na mipango ya kocha," alisema Manara.

Akizungumzia mchezo huo, Sven alisema amewataka wachezaji wake kusahau matokeo yaliyopita na kuelekeza akili zao kwenye mchezo wa leo.

Sven alisema walipata matokeo waliyostahili kwa sababu hawakupigania ushindi, hivyo leo hawana budi kuhakikisha wanashinda dhidi ya Ruvu Shooting.

"Tunapaswa kukubali na kusonga mbele, tayari nimewataka wachezaji wangu kutazama mechi inayofuata," Sven alinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >